# KUCHUNGUZA MATUMIZI YA SEMI ZILIZOANDIKWA KATIKA NYUMBA ZA VIJIJI: MFANO KUTOKA PEMBA

**MAIMUNA HAJI ALI**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SEHEMU YA MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI YA KISWAHILI (M.A KISWAHILI) KATIKA IDARA YA LUGHA NA TAALUMA ZA FASIHI YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2022**

## UTHIBITISHO

Aliyetia saini hapa chini anathibitisha kwamba ameisoma kazi hii iitwayo "***Kuchunguza Matumizi ya Semi zilizoandikwa katika Kuta za Nyumba za Vijiji: Mfano Kutoka Pemba***" na anapendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kutunukiwa shahada ya uzamili ya Kiswahili katika Idara ya Lugha na Taaluma za Fasihi ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

**Dkt. Mohamed Omary Maguo**

**(Msimamizi)**

Tarehe---------------------------------

## HAKIMILIKI

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa njia yoyote ile, iwe ama kazi nzima au sehemu ya tasnifu hii, kwa ajili ya utafiti, kujisomea au kufanya marejeo ya kitaaluma bila ruhusa ya mtafiti au kwa niaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

## TAMKO

Mimi **Maimuna Haj**i **Ali**ninathibitisha kuwa tasnifu hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa katika chuo kikuu chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada kama hii au nyingine yoyote.

----------------------------------

Saini

----------------------------------

Tarehe

## TABARUKU

Napenda kuitabaruku tasnifu hii kwa wazazi wangu, Bwana Haji Ali Haji na Bi. Saumu Ali Mjaka kwa kunilea na kunipa malezi mazuri. Pia, naitabaruku kazi hii kwa muume wangu kipenzi, Bwana Omar Issa Ali nawaombea Mwenyezi Mungu awape kila la kheria hapa Duniani na Akhera.

## SHUKURANI

Kwanza, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uhai, uzima, nguvu, fahamu na kunitatulia mitihani ya dunia iliyonikabili katika kipindi chote cha masomo yangu hadi leo nimefikia ngazi hii ya elimu. Kwa uchache wa shukurani ninasema “Alhamdulillahi.”

Pili, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa msimamizi wangu wa utafiti huu, Dokt. Omary Maguo kwa kuniongoza katika kuifanikisha tasnifu hii. Mawazo yake yalikuwa ya msingi sana hadi leo nimeikamilisha tasnifu hii. Kwa hekima na busara za dhati aliniongoza, alininasihi, alinishauri na kunikosoa kila panapostahiki bila kuchoka na kwa moyo wa thabiti. Kila hatua alitoa ushauri wa kuimarisha kazi hii hadi imekamilika. Namuomba Mwenyezi Mungu amlipe kila la kheri, Amin.

Tatu, natoa shukurani kwa uongozi mzima wa Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kuanzia makao makuu Dar es Salaam hadi tawi la Pemba. Kwa sababu hawa ni wengi na wote hao wana mchango mkubwa katika taaluma yangu ya utafiti huu. Hapa nitawataja wachache akiwemo Mwalimu Bakar Kombo Bakar, Hemed Said Massoud,Shariff Juma Faki, Dokt. Amour Rashid Ali na Nassor Suleiman Ali nao naewaombea kila la kheri.

Nne, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa familia yangu nikianzia na mume wangu mpenzi Bw. Omar Issa Ali, watoto wangu Muntar Omar Issa,Mursaynat Omar Issa, Mundhri Omar Issa, Mulhat Omar Issa,Mudriki Omar Issa na Mustamir Omar Issapamoja na ndugu zangu wote. Ninawashukuru sana kwa uvumilivu na ushirikiano walionipa katika kipindi chote cha masomo yangu.

## IKISIRI

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni “Kubainisha na kuchambua dhamira na vipengele vya lugha katika semi zinazoandikwakwenye nyumba za vijiji za Pemba.” Utafiti huu ulikuwa na malengo mahususi matatu ambapo lengo mahususi la kwanza lilikuwa ni; “Kuzianisha semi zinazopatikana katika kuta za nyumba za vijiji kisiwani Pemba.” Lengo hili liliongozwa na swali la utafiti lisemalo; “Ni semi zipi zinazopatikana katika kuta za nyumba za vijiji za Pemba?” Lengo mahususi la pili lilikuwa ni “Kubainisha matumizi ya lugha katika semi zinazopatikana katika kuta za nyumba za vijiji za Pemba.” Lengo hili liliongozwa na swali la utafiti lisemalo “Ni vipengle vipi vya lugha vinavyopatikana katika semi zinazopatikana katika kuta za nyumba za vijiji za Pemba?” Na lengo mahususi la tatu lilikuwa ni “Kutathmini dhamira zinazojitokeza katika semi zinazopatikana katika kuta za vijiji za Pemba.” Lengo hili liliongozwa na swali la utafiti lisemalo “Ni dhamira zipi zinazopatikana katika semi zinazoandikwa katika kuta za nyumba za vijiji za Pemba?” Data za utafiti huu zilikusanywakwa kutumia mbinu ya ushuhudiaji na kuchambuliwa kwa mkabala wa kimaelezo sambamba na nadharia za Simiotiki na Mwitiko wa Msomaji. Matokeo ya utafiti huu yameonesha semi ziandikwazo kwenye kuta za nyumba za vijiji za Pemba zinaweza kuwekwa katika makundi ya semi zenye kuonesha utabaka, kuhimiza mshikamano, kuonesha imani, kuhamasisha kazi, kukosoa, kukejeli, kuonesha utamaduni, mapenzi na kuifunza jamii.Kwa upande wa lugha inayotumika katika semi ziandikwazo katika kuta za nyumba za vijiji za Pemba utafiti umebainikuwa semi hizo zinatumia lugha ya lahaja, balagha, kejeli, tashihisi, misemo, methali na takiriri. Aidha, dhamira zinazopatikana katika semi hizo ni kuburudisha, kuifunza jamii, kukosoa, mapenzi, kukejeli, itikadi, uchumi, wivu na usimamizi wa haki.

**Maneno Makuu:***Kuta*, *Vijiji*, *Itikadi*

## YALIYOMO

UTHIBITISHO ........ ii
HAKIMILIKI ........ iii
TAMKO ........ iv
TABARUKU ........ v
SHUKURANI ........ vi
IKISIRI ........ vii
YALIYOMO ........ viii

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI WA JUMLA ........ 1**
1.0 Utangulizi ........ 1
1.1 Usuli wa Mada ........ 1
1.2 Tatizo la Utafiti ........ 3
1.3 Malengo ya Utafiti ........ 4
1.3.1 Lengo Kuu ........ 4
1.3.2 Malengo Mahususi ........ 4
1.4 Maswali ya Utafiti ........ 5
1.5 Umuhimu wa Utafiti ........ 5
1.6 Mipaka ya Utafiti ........ 6
1.7 Mpangilio wa Tasinifu ........ 6

**SURA YA PILI: MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA NADHARIA ........ 7**
2.1 Utangulizi ........ 7
2.2 Ufafanuzi wa Dhana ........ 7

2.2.1 Semi ........................................ 7
2.3 Vipera vya Semi ........................................ 8
2.3.1 Methali ........................................ 8
2.3.2 Vitendawili ........................................ 9
2.3.3 Mafumbo ........................................ 9
2.3.4 Misemo ........................................ 10
2.3.5 Nahau ........................................ 10
2.4 Tafiti Kuhusu Semi ........................................ 11
2.5 Pengo la Utafiti ........................................ 15
2.6 Mkabala wa Nadharia ........................................ 15
2.6.1 Nadharia ya Simiotiki ........................................ 15
2.6.2 Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ........................................ 18
2.7 Hitimisho ........................................ 21

**SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI ........................................ 22**

3.0 Utangulizi ........................................ 22
3.1 Eneo la Utafiti ........................................ 22
3.2 Usanifu wa Utafiti ........................................ 22
3.3 Kundi la Watafitiwa ........................................ 23
3.4 Sampuli na Usampulishaji ........................................ 23
3.4.1 Sampuli ........................................ 23
3.4.2 Usampulishaji ........................................ 23
3.5 Aina ya Data Zilizokusanywa ........................................ 24
3.5.1 Data za Msingi ........................................ 24

3.6 Njia za Kukusanya Data ... 24

3.6.1 Njia ya Maktabani ... 25

3.6.2 Njia ya Maskanini ... 25

3.7 Usahihi, Kuaminika kwa Data na Maadili ya Utafiti ... 26

3.7.1 Usahihi wa Data ... 26

3.7.2 Kuaminika kwa Data za Utafiti ... 26

3.7.3 Maadili ya Utafiti ... 26

3.8 Hitimisho ... 27

**SURA YA NNE: UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI ... 28**

4.0 Utangulizi ... 28

4.1 Semi Zinazoandikwa katika Kuta za Nyumba za Vijiji Kisiwani Pemba ... 28

4.1.1 Semi Zinazoonesha Utabaka ... 29

4.1.2 Semi za Umoja na Mshikamano ... 30

4.1.3 Semi za Imani ... 30

4.1.4 Semi za Kuhamasisha Kazi ... 31

4.1.5 Semi Zinazokosoa ... 32

4.1.6 Semi Zenye Kukejeli ... 33

4.1.7 Semi za Utamaduni ... 34

4.1.8 Semi za Mapenzi ... 35

4.1.9 Semi Zinazoifunza Jamii ... 36

4.1.10 Semi Zinazoonyesha Utabaka ... 37

4.2 Lugha katika Misemo Iliyoandikewa kwenye Kuta za Nyumba za Vijiji za Pemba....39
4.2.1 Matumizi ya Lahaja ....39
4.2.2 Balagha ....40
4.2.3 Kejeli....42
4.2.4 Tashihisi....42
4.2.5 Misemo ....43
4.2.6 Methali ....44
4.2.7 Takriri ....46
4.3 Dhamira Zinazowasilishwa na Semi Zilizoandikwa katika za Nyumba za Vijijiza Pemba ....47
4.3.1 Kuburudisha....47
4.3.2 Kuifunza Jamii....48
4.3.3 Dhamira ya Kukosoa....52
4.3.4 Mapenzi ....53
4.3.5 Kukejeli....55
4.3.6 Itikadi ....57
4.3.7 Uchumi....59
4.3.8 Wivu....61
4.3.9 Usimamizi wa Haki....63
4.4 Hitimisho....64

**SURA YA TANO: MUHUTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO........65**

5.1 Utangulizi....65

5.2 Muhutasari wa Tasinifu ........................................................................65

5.3 Matokeo ya Utafiti ..............................................................................67

5.3.1 Lengo Mahususi la Kwanza ..................................................................67

5.3.2 Lengo Mahususi la Pili ........................................................................68

5.3.2 Lengo Mahsusi la Tatu.........................................................................68

5.4 Hitimisho..............................................................................................68

5.5 Mapendekezo ya Utafiti .......................................................................69

**MAREJELEO…....................................................................................70**

**VIAMBATISHO .....................................................................................74**

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI WA JUMLA

## 1.0 Utangulizi

Katika sura hii mtafiti amefanya uwasilishaji wa vipengele vya utangulizi katika tasnifu hii yenye mada "Kuchunguza Matumizi ya Semi Zilizoandikwa katika Nyumba za Vijiji: Mifano KutokaPemba.Vipengele vilivyojadiliwa katika sura hii ni usuli wa mada, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti, muundo wa tasnifu na hitimisho

## 1.1 Usuli wa Mada

Semi ni kauli fupi fupi za lugha ya kifasihi ambayo kwa kawaida huwa zimebeba dhimakadhaakatika jamii.Kipacha (2014) anaeleza kuwa dhana ya semi imejumuisha tanzu nyingi za fasihi simulizi ikiwemo methali, vitendawili, mafumbo simo, lakabu na kauli tauria. Misemo kwa ujumla wake husawiri amali za jamii inayohusika. Hutumiwa na wanajamii kueleza dira na kuendeleza itikadi inayohusika na muktadha wa maendeleo ya jamii hiyo.

Pia, misemo hutumiwa na wanajamii wanapozungumza na hata katika maandishi ya miktadha mbalimbali kama vile; katika vyombo vya usafiri vya baharini na nchi kavu na hata katika kuta zikiwemo kuta za nyumba za vijiji. Nyumba hizi zilijengwa katika jamii ya Wazanzibar mara tu baada ya Zanzibar kupata uhuru ikiwa ni juhudi za kuwaweka pamoja Wazanzibar. Bw. Mohamed Ali Salim wa Kwale, ambaye ni mmoja wa wanakijijikinachopatikana nyumba za vijijianalithibitisha hilo kwa kusema kuwa nyumba za vijiji ziliopo katika kijiji cha Kwale Wilaya ya Chakechake

Pemba, zilijengwa mnamo 1978 wakati wa uongozi wa raisi wa awamu ya pili ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Mh. Aboud Jumbe Mwinyi.

Katika nyumba hizo kuna semi ambazo zimekuwa zikibeba dhamira zinazoihusu jamii. Kama tunavyojuwa kwamba dhamira ni mawazo makuu ya mtunzi katika miktadha ya kifasihi. Kama anavyoeleza Madumulla (2009) kwamba dhamira niwazo kuu katika kazi ya fasihi.Madumulla anaendelea kueleza kuwa Senkoro (1981) anatanabahisha suala la kuchanganya dhana ya dhamira na maudhui. Anasisitiza kuwa dhamira ni sehemu tu ya maudhui. Kupitia maelezo haya mtafiti amepata uelewa kwamba dhamira ni sehemu ndogo kati ya vipengele vingi vya maudhui ambavyo ni pamoja na ujumbe, falsafa ya mtunzi, mtazamo na migogoro. Kwa mantiki hii mjadala huu umemsaidia mtafiti kubainisha dhamira bila ya kuchanganya na vipengele vyengine vya maudhui.

Suala la matumizi ya lugha limewahi kufanyiwa utafiti nawatafiti wa ndani na nje ya Afrika, Tanzania ikiwemo.Wafubwa (2016) alifanya uchunguziunaohusu matumizi ya sitiari katika tamthilia za *Kivuli Kinaishi*na*Kitumbua Kimeingia Mchanga*. Katika utafiti huo Wafubwa (keshatajwa) alichunguza namna lugha ya sitiari ilivyotumiwa na watunzi wa tamthiliya teule katika kuibua ujumbe. Utafiti huo unaeleza kuwa dhamira na maudhui haviwezi kuwasilishwa vizuri bila ufundi wa lugha. Maelezo haya yana ukweli kwani lugha ndio uti wa mgongo wa kazi ya fasihi.

NayeMigodela (2017) alifanya uchunguzi wa dhamira za maandishi ya kuta za vyooni jijini Dar es Salam. Katika utafiti huo Migodela aligundua kwamba maandishi ya kuta za vyooni jijini Dar es Salam yamesawiriwa kwa usanii mkubwa

ambao umeibua dhamira za umuhimu wa elimu, dini, maadili na utamaduni kwa jumla. Kazi hii imemsaidia mtafiti kufikia lengo la utafiti huu. Migodela alitafiti dhamira katika semi kamailivyofanyika katika utafiti huu.

Aidha, Ali (2018) alifanya uchunguzi wa dhima za semi katika vyombo vya uvuvi kwa jamii ya Watumbatu. Katika utafiti huo aligundua kuwa semi hizo zina dhima ya kutunza historiana matukio muhimu ya jamii, kutambulisha chombo katika taasisi rasmi, kudokeza wasifu wa chombo, nahodha na hata mmiliki wa chombo. Pamoja na dhima hizo, majina hayo yanaendeleza fasihi ya Kiswahili. Maelezo haya yamemsaidia mtafiti kuona namna semi zinavyoibua dhamira katika jamii hasa tunapozingatia kwamba jamii jamii hizo zina mwingiliano na uhusiano katika matumizi ya semi.

Sababu iliyomsukuma mtafiti kufanya utafiti huu ni kutokana na kwamba jamii ya Wapemba ina semi ambazo zimekuwa zikiandikwa katika kuta za nyumba za vijiji hata hivyo semi hizo inaonekana hazijatiliwa mkazo katika kufanyiwa utafiti ili kubaini namna zinavyotumika na namna zinavyoibua dhamira.Utabiri wa Kezilahabi (1988) unaonesha kuwa nyakati zitafika ambapo misemo yaKiswahilihaitakuwa vyombo vya kuasa na kujenga jamii tu, bali pia zitatumika katika utatuzi wavikwazovya hali ya maisha. Kutokana na muktadha huo utafiti huu umefanyika ili kuona namna semi hizo zinavyotumiwa na wanajamii ili kuibua dhamira mbalimbali zinazoihusu jamii na namna vipengele vya lugha vinavyotumika katika semi hizo.

## 1.2 Tatizo la Utafiti

Semi ni kauli fupi fupi zenye maonyo na maaso ndani yake (Mulokozi, 1996). Semi huwa zinatumika katika mawasiliano ya kila siku kati ya watu wa rika tofauti. Tafiti

kadhaa zimewahi kufanyika zikiwa na lengo la kuchunguza matumizi ya semi ama fani katika vipengele vya semi. Baadhi ya wale ambao wamewahi kutafiti utanzu huu ni pamoja na King`ei (2007). Kipacha (2014), Juma (2016), Hassan (2017), Migodela (2017), Oyindana Mukhwana (2017), Ali (2018) na Skuni (2018). Ni kweli kwamba semi zilizojitokeza katika vyanzo mbalimbali zimewahi kufanyiwa utafiti. Wapo watafiti kama vile Kipacha (2014),Juma (2016) na Migodela (2017)waliotafiti fani na dhamira za semi zilizoandikwa kwenye daladala, kuta za vyoo, fulana zivaliwazo kwenye taasisi fulani au hata kwenye jamii kwa ujumla, vyombo vya usafiri wa baharini, magari ya abiria na mizigo, duka za biashara na vyanzo vyengine. Pamoja na ukweli kuwa semi zimefanyiwa utafiti na watafiti wengi, utalii uliofanywa na mtafiti umebaini kuwa semi zinazoandikwa kwenye kuta za nyumba za vijiji Kisiwani Pemba bado hazijatafitiwa ili kubaini dhamira na vipengele vya lugha vinavyotumika. Kwa muktadha huo tatizo la utafiti huu lilikuwa nikutaka kubaini dhamira zinazopatikana katika semi hizo na kubaini vipengele vya lugha vinavyotumika katika semi hizo. Hivyo basi, kukamilika kwa utafiti huu kumeziba pengo hili la kitaaluma katika fasihi ya Kiswahili.

## 1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu una lengo kuu na malengo mahususi yafuatayo:

### 1.3.1 Lengo Kuu

Kubainisha nakutathmini dhamira na vipengele vya lugha katika semi zilizoandikwa katika kuta za nyumba za vijiji vya Pemba.

### 1.3.2 Malengo Mahususi

Utafiti huu ulikuwa na malengo mahususi yafuatayo:

i. Kuziainishasemi zinazopatikana katika kuta za nyumba za vijiji za Pemba.
ii. Kubainisha matumizi ya lugha katika semi zinazopatikana katika kuta za nyumba za vijiji za Pemba.
iii. Kutathminidhamira zinazojitokeza katika semi zilizoandikwa katika nyumba za vijiji za Pemba.

## 1.4 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali ya utafiti yafuatayo:

i. Ni semi zipi zilizoandikwa katika nyumba za vijiji za Pemba?
ii. Ni matumizi yepi ya lugha yaliyomo katika semizinazopatikana katika kuta za nyumba za vijiji vya Pemba?
iii. Ni dhamira zipi zinazojitokezakatika semi zinazopatikana katika nyumba za vijiji za Pemba?

## 1.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu una umuhimu ufuataao:

**Kitaaluma:** utafiti huu utawasaidia wanafunzi, walimu, wahadhiri, watafiti na hata wasomaji wa kawaida wa kazi za fasihi, kupata marejeleo muhimu yanayohusu semi.

**Kijamii**: utafiti huu utaisaidia jamii kujua kwa namna gani semi zilizoandikwa katika kuta za nyumba za vijiji kisiwani Pemba zinavyotumia vipengele vya lugha na namna semi hizo zinavyoibua dhamira katika jamii.

**Kiutamaduni:** Kwa vile utafiti huu umehusu dhamira na lugha katika semi za nyumba za vijiji katika jamii ya Wapembani wazi kwamba utawasaidia wanajamii

katika masuala yanayohusu utamaduni kama vile mapenzi. Hivyo kwa kupitia vipengele hivyo tunaona namna jamii inavyosawiriwa katika maisha ya kila siku.

## 1.6 Mipaka ya Utafiti

Kazi kuhusu semi za lugha ya Kiswahili zimewahi kufanyiwa tafiti na watafiti wengi waliotangulia. Tafiti hizi zilifanyika hapa Pemba na kwingi kwengineko. Wapo waliotafiti semi zilizoandikwa kwenye mikoba, wapo waliochunguza semi zilizojitokeza kwenye makawa, wapo waliochunguza semi zilizoandika kwenye vyombo vya usafiri; iwe daladala, gari za abiria na hata gari za mizigo. Aidha, zipo tafiti zilizochunguza semi zilizoandikwa kwenye kuta za vyoo, fulana zinazohusika na taasisi na hata fulana zinazovaliwa na wanajamii kwa jumla. Mtafiti wa kazi hii alijikita kuchunguza dhamira na matumizi ya lugha katika semi zilizoandikwa kwenye kuta za nyumba za vijiji kisiwani Pemba. Hii ni kusema kwamba mtafiti hakujishughulisha na semi za aina hii nje ya kisiwa cha Pemba na nje ya miktadha ya nyumba za vijiji. Aidha utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Simiotiki na Mwitiko wa Msomaji.

## 1.7 Mpangilio wa Tasinifu

Tasinifu hii ina jumla ya sura tano ambapo sura ya kwanza ni utangulizi ikihusisha vipengele vyote muhimu vya kiutangulizi ambavyo ni pamoja usuli, tatizo la utafiti na malengo ya utafiti miongoni mwa vipengele vingine. Sura ya pili inahusu mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia na sura ya tatu ni mbinu za utafiti. Sura ya nne inahusu uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti na sura ya tano ni hitimisho, muhtasari na mapendekezo.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA NADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Katika sura hii mtafiti amefanya ufafanuziwa maandishi ya watanguliziwaliowahi kuandika ama kufanya utafiti kuhusu mada iliyotafitiwa. Pia, katika sura hii kumebainishwa pengo la utafiti ambalo lilikusudiwa kuzibwa na utafiti huu. Mwisho sura hii imefanya uwasilishaji wanadharia ya Simiotiki na Mwitiko wa Msoamji ambazo zimeongoza utafiti huu.

## 2.2 Ufafanuzi wa Dhana

Katika sehemu hii mtafiti amefanya ufafanuzi wa dhana zinazohusiana na mda iliyotafitiwa. Dhana hizo nisemi na vipera vya semi.

### 2.2.1 Semi

Semi ni kauli fupifupi ambazo huelezwa kimafumbo. Mulokozi (1996) anaieleza dhana ya semi kwamba ni kauli fupi fupi zenye maonyo na maaso ndani yake. Naye Simiyu (2011) anaeleza kuwa semi huwa ni fungu la maneno ambalo huwa fupi linalotumia ishara, picha na tamathali za semi kwa ufundi wa hali ya juu. Anavibainisha vipera vya semi kuwa nimethali, vitendawili, vitanza ndimi, misimu, misemo/nahau, mafumbo/chemshabongo, lakabu na mikatale.

Kwa ujumla baada ya kupitia maelezo ya Mulokozi (kashatajwa) na Simiyu (kashatajwa) inaweza kuhitimishwa kwamba semi ni kauli fupifupi za kisanaa ambazo hutumia lugha ya mafumbo, picha na ishara ili kufumbata ujumbe uliokusudiwa. Ili kupata ujumbe uliomo katika semi lazima mtu afanye uchambuzi

wa kina juu ya mafumbo hayo. Aidha tumebaini kuwa semi ina vipera vingi ndani yake. Vipera hivyo ni pamoja na methali, vitendawili, misemo, nahau, simo na mafumbo.

## 2.3 Vipera vya Semi

Waandishi kadhaa wamefanya ufafanuzi wa vipera vya semi. Mulokozi (1996), Simiyu (2011), Ndungo na Mwai (1993), Njogu na Chimerah (1999) na Taasisi ya Elimu Tanzania (1983) wamewahi kubainisha vipera vya semi ambavyo ni pamoja na methali, vitendawili, nahau, mafumbo, semi na simo. Kwa ujumla vipera hivi vya semi vimeelezwa na waandishi hawa kama ifuatavyo:

### 2.3.1 Methali

Methali ni semi fupi zenye mpangilio maalumu wa maneno ambazo huelezwa kwa muhutasari na kuibuwa mawazo mazito yanayotokana na uzoefu wa kijamii.Simiyu (2011) anasema kuwa methali ni semi fupi zinazosheheni fumbo juu ya ukweli wa maisha ya binadamu na huwa na umbo maalumu. Semi hizi kwa kawaida huwa za kimapokeo kutoka kizazi hadi kizazi. Kimuundo methali huwa na sehemu mbili ambapo sehemu ya kwanza huzua suala na sehemu ya pili hukamilisha wazo. Aidha, methali huwa na lugha teule inayojumuisha sitiara, nidaa, tashibiha, taswira, balagha, mchezo wa maneno na tanakali za sauti.

Katika utafiti huu methali inaweza kuelezwa kuwa ni usemi mfupi ambao huwa ni tegemezi, yaani upande mmoja huanzisha wazo na mwengine hukamilisha wazo. Pia, methali huweza kutumia wahusika wanyama, vitu au watu kama ni ishra ya kufumbata dhamira zilizokusudiwa. Vile vile, ikumbukwe kwamba muundo wa semi

za Kiswahili hubakia kuwa wa jadi na hauwezi kubadilishwa bila ya kupoteza uasili unaozoeleka na jamii husika.

### 2.3.2 Vitendawili

Vitendawili ni aina ya maswali yanayotumia sana lugha ya picha ili kufanya yawe mafupi. Ndungo na Wafula (1993) wanasema kwamba vitendawili ni moja wapo ya tanzu za fasihi simulizi. Zaidi ya hayo vitendawili ni kauli fupi fupi zenye mafumbo ambayo hudai ufumbuzi. Fumbo lenyewe huwa ni kauli ambayo huwa na maelezo ya kutega na hivyo hudai uteguzi. Hii ni kusema kwamba vitendawili ni mafumbo ambayo ufumbuzi wake huwa ni wa kidrama kwani huwakusanya fanani na hadhira huku kila mmoja kati ya hadhira na fananikushiriki kutoa maelezo kutegemea kitendawili husika. Kwa mfano:

A: Kitendawili

B: Tega

A: Tega ni kutege.

B: Jawabu lake ni "mwiba."

Katika mfano wahapo juu mhusika "A" anafumba fumbo na mhusika "B" anapata nafasi ya kulifumbua fumbo hilo. Iwapo mhusia "B" atashindwa kulijua jibu la fumbo hilo, atatoa mji na hivyo kutoa fursa kwa "A" kutoa jibu la kitendawili hicho.

### 2.3.3 Mafumbo

Mafumbo ni semi au kauli za maonyo au mawaidha zenye maana iliyofichika. Mafumbo hutolewa kwa kuficha ili kuwakilisha walengwa. Mafumbo hubuniwa kwa shabaha na kwa ajili ya hadhira maalumu. Kwa mujibu wa Mulokozi (1996)

mafumbo huficha maana na yako ya aina nyingi lakini yaliyomaarufu nimafumbo jina na mafumbo ya chemshabongo.Kwa ufafanuzi huu mafumbo yanaweza kuelezwa kuwa ni semi amabzo maana zake huwa zimefichika.

### 2.3.4 Misemo

Misemo ni mafungu ya maneno yanayotumiwa na jamii kwa namna maalumu ili kutoa maana inayoafiki ukweli fulani. Misemo hueleza maana ya kauli moja. Misemo hutumia maneno ya kawaida lakini yenye hoja au maana maalumu. Mfano (a) akili ni mali (b) mtu ni utu (c) kufa kufaana (Kaduguda, Kiango, Ipara 2015 katika Skuni, 2017). Maana hii inatupa uelewa kwamba misemo ni kauli ambazo huweza kuzushwa na kubeba ujumbe maalumu. Hata hivyo, kwa kawaida misemo huwa na ujumbe maalumu unaoshadidiwa. Kwa mfano; "elimu ni nuru" msemo huu unalenga kutilia mkazo umuhimu wa elimu katika maisha ya kila siku. Aidha, "maji ni uhai," ni msemo wenye lengo la kuonesha umuhimu wa maji.

### 2.3.5 Nahau

Ni lugha ambayo maana yake huwa imefichwa. Hivyo, hata misemo huweza kuwa nahau. Wamitila (2010) na Simiyu (2011) wanaeleza kuwa uchanganuzi wa nahau hautegemei maana maalumu za maneno yaliyomo kwenye kifungu kinachounda nahau hizo bali hutegemea maana zinazoeleweka na watumiaji kutokana na kujifunza au uzoefu walionao. Mtumiaji wa lugha anapokutana na nahau ambayo haijui maana yake kutokana na uzoefu wake kama mzungumzaji au mtumiaji wa lugha fulani au muktadha wake wa kimatumizi atashindwa kupata maana iliyokusudiwa.

Pia, Wamitila (2010) anasema kwamba lugha ya kawaida huwa na misemo na semi nyingine ambazo maana zake za kitamathali ni tofauti na maana zake za kijuujuu za misemo wenyewe. Sifa moja ya nahau ni kuwepo kwa sitiari. Kimsingi, sitiari ni nguzo kubwa katika ukuaji wa nahau. Wamitila anaongeza kuwa inawezekana lugha ya kinahau wakati fulani iliwahi kuwa lugha ya `kisitiari` lakini ule usitiari ukapotea yaani msomaji hauwazii tena bali huziona nahau weneyewe kama suaula fulani la kifomula au sitiari chakavu. Kwa mfano; nahau kamavile; mwaga unga, gonga ukuta, ingia mitini, pandikizi la mtu, tia masikio pamba, kuwa waya, na toa chai. Wamitila anadai kwamba tunapokumbana na nahau zilizotajwa hapa hatuwazii kwamba zina sifa za sitiari ambapo katika mfano wa wa kwanza "kazi" inafananishwa na "unga." Hivyo uchanganuzi wa sifa hizi hauwezi kujifunga kwenye semi tu zinazokubalika katika muktadha rasmi yaani nahau, misemo na methali bali lazima kuchunguza matumizi ya michuuko na simo.

Hivyo basi, katika utafiti huu nahau imeelezwa kuwa ni matumizi ya lugha ambayo maana yake huwa imejificha. Ili kupata maana hiyo lazima iwe kwa uzoefu mkubwa unaotokana na watumiaji wa lugha husika. Kwa kawaida maana hizo huwa tata kwani huweza kuwatatiza hata wazawa wa lugha.

## 2.4 Tafiti Kuhusu Semi

Tafiti kadhaa zimewahi kufanyika kuhusu semi. Juma (2008) aliandika makala yenye mada *"Kiswahili cha Asili cha Kina Mama wa Visiwani Zanzibar."*Katika utafiti huo kunaelezwa kuwa kina mama wa Zanzibar wanapenda kutumia semi, nahau, mafumbo, vitendawili na maneno ya hekima. Semi mbalimbali hutumika kwa madhumuni tofauti, kama kuonya, kuasa, kufunza, kuonesha dharau, kejeli, hasira,

kuthibitisha au kukazia jambo ambalo limetangulia kusemwa.Kwa sababu hiyo, utanzu wa semi huwa ni maarufu sana katika Visiwa vya Zanzibar. Utafiti huu ulikuwa na umuhimu katika kufikia malengo ya utafiti. Hii inatokana na ukweli kwamba vipengele vya semi vilivyotafitiwa na Juma vimejitokeza katika utafiti huu ingawa kwa miktadha tofauti. Pia, kupitia utafiti huo mtafiti amejifunza namna ya kuzitafiti data zinazotokana na semi kwa msingi wa kisayansi. Kwa mantiki hiyo, utafiti huo ulikuwa ni kielelezo cha marejeo wakati wa kuwasilisha data katika sura ya nne ya utafiti huu.

Utafiti mwengine ni ule uliofanywa na Juma (2015) ambao ulikuwa na mada "*Methali za Kiswahili Zilizoachwa: Sababu na Athari zake kwa Jamii."* Matokeo ya utafiti huu yalionesha kuwa zipo methali za Kiswahili zilizoachwa. Pia zipo methali zinazotumiwa sana na nyengine kwa nadra. Sababu za kuziacha methali hizo ni maendeleo ya sayansi na teknolojia, ukosefu wa taasisi za kuzihifadhi na kuzirithisha, mabadiliko ya msamiati uliotumika katika methali hizo na kuibuka kwa methali nyingi mpya. Utafiti huu pia umekuwa na manufaa katika kukamilisha malengo ya mtafiti. Kwa vile methali ni moja kati ya vipengele vya semi, mtafiti amebaini namna ya kuvifanyia uchambuzi vipengele hivyo kwa mkabala wa kifasihi. Pia, utafiti huo ulizibainisha methali kutegemea sifa mahususi, hivyo mtafiti kupitia utafiti huo amejifunza namna semi zinavyoweza kubainishwa kama sehemu ya data za utafiti. Kwa hivyo, ilikuwa rahisi kwa mtafiti kufikia lengo la utafiti linalohusu kubainisha semi za kwenye nyuumba za vijiji.

Naye Migodela (2017) alifanya uchunguzi wa dhamira za maandishi ya kuta za vyooni jijini Dar es Salam. Katika utafiti huo Migodela aligundua kwamba

maandishi ya kuta za vyooni jijini Dar es Salam yamesawiriwa kwa usanii mkubwa ambao umeibua dhamira za umuhimu wa elimu, dini, maadili na utamaduni kwa jumla. Utafiti huu umeingia ndani zaidi na umelandana na baadhi ya malengo ya utafiti uliofanyika. Katika utafiti huo mtafiti amejifunza namna ya kuzielezea dhamira za semi na namna matumizi ya lugha yanavyoweza kufanyiwa ufafanuzi katika semi za Kiswahili. Tofauti ya utafiti wa Migodela na utafiti huu ni kwamba yeye alichunguza maandishi ya kuta za choo za jijini Dar es Salam wakati katika utafiti huu mtafiti alichunguza maandishi ya kwenye kuta za nyumba za vijiji katika jamii ya Pemba.

Utafiti mwengine uliojikita kuchunguza matumizi ya lugha ni ule wa Ibrahim (2017)ambaye alifanya utafiti wenye mada *Uchunguzi wa Matumizi ya Lugha katika Matangazo ya Biashara.*Utafiti huo ulichunguza namna vipegele vya lugha ya kiisimu pamoja na vile visivyokuwa vipengele vya lugha ya kiisimu kama matumizi ya rangi, picha na michoro nakadhalikavinavyojidhihirisha katika matangazo ya biashara.Matokeo ya utafiti huo yalionesha kuwa lugha ina thamani katika mawasiliano hususani katika matangazo ya bidhaa na huduma. Thamini ya lugha katika matangazo ya biashara iko sambamba navitu vyengine kama vile picha, michoro nakadhalika. Vipengele hivi hukidhi haja ya kibiashara kutokana nakumvutia mnunuzi. Ingawa utafiti huu ulijikita katika maandishi ambayo hayako katika kuta, lakini maandishi yaliyotafitiwa yamempa uelewa mtafiti namna ya kutafiti vipengele vya lugha na namna vinavyoweza kubeba dhima mbalimbali ikiwemo ile ya kuonesha dhamira.

Pia, kuna utafiti uliofanywa kuhusu semi zilizoandikwa katika vyombo vya baharini. Utafiti huo uliofanywa naAli (2018) ambapo alifanya uchunguzi wa dhima ya majina

katika vyombo vya uvuvi kwa jamii ya Watumbatu. Katika utafiti huo aligundua kuwa majina hayo yana dhima ya kutunza historia na matukio muhimu ya jamii, kutambulisha chombo katika taasisi rasmi, kudokeza wasifu wa chombo, nahodha na hata mmiliki wa chombo. Pamoja na dhima hizo, majina hayo yanaendeleza fasihi ya Kiswahili. Utafiti huu pia ulionesha namna semi zinavyoibua dhima zinazohusu jamii. Aidha, utafiti ulizipanga data kulingana na sifa za semi hizo. Kwa mantiki hiyo, katika utafiti huu mtafiti alipata uelewa wa namna ya kuziwasilisha data hizo na hatimae kufikia hitimisho.

Utafiti kuhusu semi pia umewahi kufanywa naSovu (2018) akiwa na mada *Matumizi ya Tamathali za Semi za Kiswahili katika Kampeni za Kisiasa: Mifano katika Uchaguzi wa Tanzania wa 2015*. Katika utafiti huo kulibainika kuwa wanasiasa walikuwa wakitumia tamathali za semi za sitiari, kinaya, mdokezo, taashira, taniaba, tashibiha, tashihisi, tashititi na tafsida ili kushawishi, kuwaamsha wasikilizaji, kuwazindua, kuwavuta katika chama chao, kuwabembeleza, kuwadhoofisha wagombea wa vyama vingine na kuonyesha mshikamano wa kijamii.

Utafiti huu ingawa ulijikita katika lugha inayotumika katika miktadha ya kisiasa napia ulikuwa na kasoro ya kuvibainisha vipengele ambavyo si tamathali za semi kama vile; mdokezo, taniaba na tashititi, lakini ulikuwa na faida katika kuyafikia malengo ya utafiti huu. Kwanza, mtafiti amepata uelewa wa namna ya kufanya uchambuzi wa vipengele vya lugha vinavyojitokeza katika tamathali za semi. Pia, mtafiti amebaini kuwa kila semi inatumiwa na wanajamii ikiwa na lengo mahususi. Kwa mantiki hiyo, utafiti huu uliyachukua mawazo hayo kamasehemu ya uchambuzi, uwasilishaji na kujalizishia data zilizokusanywa.

## 2.5 Pengo la Utafiti

Mtafiti ametalii machapisho kadhaa yanayohusu mada iliyotafitiwa. Machapisho hayo yamejikita kufanya uchunguzi wa vipera mbalimbali vya semi kwa mkabala wa fani na maudhui kama sehemu ya fasihi. Hata hivyo hakuona kazi iliyowahi kufanyika ikiwa na lengo la kuchunguza matumizi ya vipengele vya lugha na dhamira katika semi zinazoandikwa kwenye kuta za nyumbaza vijiji katika kisiwa cha Pemba. Hivyo basi, aliona ipo haja ya kufanya utafiti huu kwa vile jamii hiyo imekuwa ikitumia semi hizokatika maisha yao ya kila siku.

## 2.6 Mkabala wa Nadharia

Nadharia inaweza kuelezwa kuwa ni mawazo ya kina yaliyofanyiwa uchunguzi ili kuweza kutumika katika jambo fualani. Wakieleza kuhusu dhana ya nadharia Njogu naChimerah (1999), Wafula (2007) na Sengo (2009) wanamawazo yanayofanana ambapo wanasema nadharia ni wazo kuu, fikra kuu, muongozo mkuu, wa mtu au jamii wa pahala fulani, wakati fulani, kwa sababu fulani. Aidha, wanaendelea kueleza kuwa nadharia ni miongozo inayo muelekeza mtafiti wa kazi ya fasihi ili kufikia lengo analolikusudia. Nadharia inatufanya tufikiri, tusaili, tuweke tashwishi na tuone ukweli. Nadharia inatoa muangaza na kuweka wazi kilichojificha.Katika utafiti huumtafiti aliongozwa na nadharia ya Simiotiki na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji. Ufafanuzi wa nadharia hizi ni kama ufuatao:

### 2.6.1 Nadharia ya Simiotiki

Wamitila (2002) anaeleza kuwa Simiotiki ni neno la lugha ya Kiyunani lenye maana ya ishara na ambalo linatumika kueleza mielekeo na makundi fulani ya kihakiki. Makundi hayo na mielekeo hiyo imezuka na mtindo wa kuzihakiki kazi za kifasihi

ambapo unaangaza ishara katika kazi hizo. Kuzuka kwa nadharia hii kunahusishwa kwa kiasi kikubwa na miaka ya 1970. Wakati huo kulikuwa na mwelekeo mkubwa wa kuuasi na kuuwacha umuundo ambao ulikuwa umeutawala uhakiki wa kifasihi katika miaka ya 1960. Nadharia hii inahusishwa na mawazo ya mwanaisimu wa Kiswizi, aliyejulikana kwa jina la Ferdinand de Saussare ambaye inasemekana ndie mwanzilishi wa nadharia hii na aliungwa mkono na mwanafalsafa wa Kimarekani aliyejulikana kama Charles-Pierce ambaye nae anahusishwa na kielelezo cha ishara kinachohusishwa na pembe tatu ambazo ni ishara, yambwa  na kifasiri. Kwa mujibu wa mwanafalsafa huyu kila ishara huwa yambwa au kitendwa kinachorejelewa.

Kifasiri ni kile kinachochochewa katika akili ya anayeifasiri ishara hiyo. Kimsingi tunaweza kusema hii ni nadharia inayoshughulika na ishara na uashiriaji katika kazi za kifasihi. Mwelekeo mkubwa wa nadharia hii kupendelea neno matini unawafanya baadhi ya wahakiki kuiita nadharia ya umatini (textuality). Baadhi ya wahakiki hupendelea neno Semiolojia badala ya Simiotiki. Suala la ishara na uashiriaji kama anavyoelezea Culler limeanza kuwa muhimu katika uhakiki wa kifasihi wa miaka ya sabiini.

Sambamba na hilo, mwanafalsafa huyu amekuwa mhakiki muhimu katika kuweka misingi mikuu ya nadharia hii. Mawazo yake pamoja na Julia Kristeva yameacha athari kubwa katika uhakiki wa ishara na uashiriaji katika kazi za kifasihi. Dhana moja muhimu iliyohusishwa na Barthes ni msimbo. Kwa mujibu wa mawazo ya mtaalamu huyu, kila leksia hudhihirishwa misimbo au kaida fulani ambazo huwa muhimu katika kuifasiri.

**Misimbo ya Nadharia ya Simiotiki**

Barthes (1994) anaeleza kwamba kuna aina tano za misimbo inayotumika katika kazi za fasihi ambazokwa pamoja huunda nadharia ya Simiotiki. Aina hizo ni msimbo wa kimatukio, msimbo wa kihenemetiki, msimbo wa ki-seme, msimbo wa kiishara na msimbo wa kiurejelezi. Nadharia ya Simiotiki haiwezi kukamilika bila ya kurejelea mawazo ya Barthes kuhusu misimbo mitano ya usomaji ambayo ni miongoni mwa mihimili mikuu ya nadharia hii. Mtaalamu huyu anafafanua misimbo hiyokama ifuatavyo:

**Msimbo wa Kimatukio**: Huu unahusisha jinsi msomaji anavyounda na kuuelewa msuko wa kazi hiyo kwa kuangalia jinsi matukio hayo yanavyofuatana kiathari au kisabasishi.

**Msimbo wa Kihemenetiki**: Huu nao unahusu taharuki na unajulikana na baadhi ya wahakiki kama msimbo wa kusimulia au kutamka hadithi. Msimbo huu unaweza kufumbatwa kwenye anuani ya kazi za kifasihi.

**Msimbo wa Ki-seme**: Msimbo huu unahusiana na jinsi msomaji atakavyoishia kuipata picha ya mhusika fulani wa kifasihi.

**Msimbo wa Kiishara**: Huu ni msimbo muhimu katika usomaji na uhakiki wa kazi za kifasihi. Msimbo huu unahusishwa na jinsi ambavyo wasomaji wanavyovumbua maana ya kiishara katika kazi za kifasihi.

**Msimbo wa Kiurejelezi**: Msimbo huu unajengwa kutokana na viashiria vya utamaduni unaorejelewa katika kazi inayohusika. Urejeshi huu huunda uhalisi

mahususi kutokana na matumizi ya vitu fulani vinavyoeleweka na wasomaji na kwa njia hiyo huipa kazi fulani nguzo ya kitamaduni.

Nadharia ya Simiotiki ingawa inakosolewakwa mapungufu ya kujikita zaidi kuchunguza vipengele vya fani na kuitenga maudhui lakini mtafiti aliona kuwa inafaa kumuongoza kufikia lengo la pili la utafiti huu linalohusu kubainisha vipengele vya lugha vinavyojitokeza katika semi za majumba katika jamii ya Wapemba. Kwa sababu nadharia hii inajikita zaidi kutathmini vipengele vya lugha, mtafiti ameichagua nadharia ya Mwitiko wa Msoamji ili kutumika katika lengo la kwanza na la tatu la utafiti huu. Nadharia hiyo imefanyiwa ufafanuzi kama ifuatavyo:

### 2.6.2 Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji

Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji inajadiliwa na Wamitila (2002) kuwa ni nadharia inayorejelea mitizamo au tabia fulani za usomaji wa matini zinazohusisha uhakiki wa aina mbalimbali ambao huchunguza dhima na majukumu ya msomaji katika matini au kazi za fasihi.Waasisi na watetezi wa nadharia hii ni Fish (1980), Tompkins (1980) na Wolfgang (1974).

Lengo la msingi la nadharia hii ni kuwabainisha wasomaji, kuwachunguza pamoja na tendo zima la usomaji.Wahakiki wanaojishughulisha na nadharia hii wanaelekea kuwa na mtazamo tofauti na ule wa kijadi wa kuiangalia fasihi kama kitu kilichokamilika. Hawa wanaamini kuwa, maana yeyote ya kifasihi inategemea kwa kiasi kikubwa msomaji wa kazi hiyo. Msomaji husawiriwa kama mwenye mchango mkubwa katika kubuni maana ya kazi husika ya fasihi. Hii ni sawa na kusema kuwa

si rahisi kudai kuwa kuna maana fulani sawa na sahihi zaidi ya kazi fulani ya kifasihi kwa msomaji.

Wasomaji wanaweza kuvifasiri vipengele vya kiisimu na kisanaa kwa namna mbalimbali.Tofauti hizo za maana huweza kusababishwa na vipengele mbalimbali vya kimsingi vinavyounda mwitiko wa msomaji. Tofauti kati ya matini husika na hisia za kibinafsi za msomaji anayehusika na utofauti wa namna matini inavyoelekeza au kutatiza.Sifa hiyo ni ile inayowezesha kuwepo kwa maana au fasili mbalimbali za kazi moja ya fasihi. Kimsingi tunakubaliana na mawazo ya nadharia hii kwani yanampa msomaji uhuru wa kuweza kuisoma, kuielewa na kuihakiki kazi ya fasihi kwa kadri ya uelewa na tajriba ya msomaji husika kuhusu masuala mbalimbali ya kijamii. Wafula (2007) anaeleza kuwa waitifaki wa nadharia hii huuliza maswali ambayo kwayo huibua misingi ya nadharia hii.Maswali yanayoulizwa ni:-

a) Kuna uwiano wowote kati ya maana inayosomwa na jinsi msomaji anavyoihakiki?

b) Je, kazi ya fasihi ina maana kufuatana na msomaji binafsi na jinsi anavyoichukulia?

c) Kuna wasomaji ambao husoma na kutafsiri kazi za fasihi vizuri zaidi kuliko wasomaji wengine?

d) Msomaji hutumia vigezo gani kujijulisha iwapo mawazo yake juu ya kazi fulani yanafaa au hayafai?

Adena (1971) anadai kuwa kazi ya fasihi ni kama kinyago ambacho hakijakamilika na kwa hivyomchongaji hujaribu kukikamilisha. Kwa hivyo mhimili wa kwanza wa nadharia hii ni kwamba:

1. Msomaji huikamilisha kazi ya sanaa kwa kuijaliza kwa usomaji makini au kuidhalilisha kwa usomaji wa kiholela.
2. Nadharia hii inasisitiza athari za kazi za fasihi juu ya akili na maarifa ya mwandishi.

Wasomi mbalimbali hufasiri athari hizo kupitiaa njia tofauti tofauti kutegemea:

i. Tofauti kati ya matini na hisia za kibinafsi za msomaji.
ii. Namna matini inavyoelezea au kutatiza mwitiko wa msomaji.Sifa inayozua usomaji mzuri au mbaya wa kazi inayohusika.

3. Wananadharia hawa wanashikilia kuwa kuna njia mbili za kusoma kazi ya fasihi ambazo ni:-

i. Njia inayofafanua na kusisitiza mawazo ambayo kitambo yamejulikana na kutambuliwa na msomaji.
ii. Kuwasilisha kazi ya fasihi kimafumbo ili kuchochea msomaji kujitafutia na kujiamulia ujumbe uliomo katika kazi anayoisoma. Kwa hivyo, mafumbo hayo yanapaswa kusomwa mara kadhaa ili msomaji aelewe matini anayoisoma.

4. Usomaji ni tendo linalofanyika na kutekelezwa kwa wakati maalumu, kwamba wakati wa kusomwa kwa matini huathiri sana maana ya matini hiyo.Fish anadai kwamba wasomaji wanapaswa kufanya mikabala ya aina fulanina matini hizi katika miktadha mbalimbali.

5. Msomaji anayetumia mkakati wa mwitiko kusoma kazi ya sanaa hufuata hatuatatu katika weledi wa kazi ya fasihi.
   i. Hurejelea kazi inayosomwa kwa kutafsiri ili ithibitishwe kwamba kazi hiyo inaafikiana na yale yanayokumbukwa na msomaji.
   ii. Hubainisha jinsi miktadha ya matini isiyohusiana moja kwa moja na maandishi inavyoweza kuhusishwa na kutenganishwa na msomaji.
   iii. Hudhihirisha kuwa maoni ya msomaji yanafungamana na mada muhimu za hadithi.
6. Nadharia hii inazingatia usomaji, msomaji na upokezi.

Nadharia hii ilionekana kuwa inaweza kufikisha lengo la utafiti huu. Sababu kubwa ni kwamba lengo la tatu la utafiti huu lilijikita kutathmini dhamira katika semi zinazoandikwa kwenye kuta za nyumba za vijiji za Pemba. Kwa hiyo kwa kutumia nadharia hii mtafiti amefanikiwa kuziba pengo linalotokana na mapungufu ya nadharia ya Simiotiki ya kujikita kwenye vipengele vya lugha.

## 2.7 Hitimisho

Katika sura hii mtafiti alifanya ufafanuziwa machapisho ya waandishi watangulizi ambao waliwahi kushughulikia vipera vya semi. Pia, katika sura hii mtafiti amebainisha pengo la utafiti na mwisho amefafanua nadharia ya Simiotiki na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ambazo zimeongoza utafiti huu. Sura inayofuata inahusu mbinu za utafiti zilizotumiwa na mtafiti hadi utafiti huu kukamilika.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.0 Utangulizi

Katikasura hii mtafitiamebainishambinu zilizotumika kukusanya data. Mbinu hizo ni eneo la utafiti, usanifu wa utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, data na aina za data, uchambuzi wa data, usahihi wa data za utafiti, kuaminika kwa data na maadili ya utafiti na Hitimisho.

## 3.1 Eneo la Utafiti

Eneo la utafiti ni eneo ambapo mtafiti atakusanya data. Enon (1998) anaeleza kuwa eneo la utafiti ni sehemu ambayo mtafiti huenda akiwa na lengo la kukusanya data alizozikusudia. Hivyo basi, katika utafiti huu eneo la utafiti ni semi zilizoandikwa katika kuta za nyumba za vijiji za Pemba ambazo zinapatikana katika Wilaya ya Chake chake na Wilaya ya Wete Pemba: kijiji cha Wawi, Pujini, Kengeja, Muambe, Mkoroshoni, Machomane, Mchangamdogo, Kiungoni na Mibrani.

## 3.2 Usanifu wa Utafiti

Utafiti huu umetumia mkabalawa kimaelezo. Mkabalawa kimaelezo ni ule ambao hutumia maelezo katika kuwasilisha na kuchambua data za utafiti na mkabala wa kitarakimu ni ule unaotumia nambari katika kuwasilisha na kuchambua data za utafiti. Kama anavyoelezaEnon (1998) kwamba mkabalawa kimaelezo ni njia ya ukusanyaji na uchambuaji wa data kwa njia ya maelezo, ambapo nambari huwa hazitumiki, utafiti huu data zimewasilishwa na zimechambuliwa kwa mkabala wa maelezo. Mkabala huo umeteuliwa na mtafiti kutumika katika utafiti huu kutokana

na kwamba utafiti huu ni wa kifasihi ambao unajikita kufanya uchambuzi wa sanaa ya maneno.

### 3.3 Kundi la Watafitiwa

Kothari (2014) anaeleza kuwa kundi la watafitiwa ni jumla ya kundi lote ambalo linatarajiwa kutafitiwa. Hivyo katika utafiti huu kundi la watafitiwa ni semi zote ambazo zimeandikwa kwenye kuta za nyumba za vijiji za Pemba. Kundi hilo lilitafitiwa kwa sababu hakukuwa na utafiti ambao ulijikita kutafiti eneo hilo kwenye nyumba za vijiji katika vipengele vya lugha na dhamira.

### 3.4 Sampuli na Usampulishaji

Katika sehemu hii mtafiti ameeleza sampuli iliyotumika katika utafiti huu na namna sampuli hiyo ilivyopatikana.

#### 3.4.1 Sampuli

Sampulini idadi ndogo kutoka kundi linalotafitiwa. Kothari (2014) anaeleza kwamba sampulinisehemu ya watu ama vitu vinavyotafitiwa ambavyo vinapatikana kutoka kundi kubwa la watu ama vitu hivyo. Sehemu hiyo huteuliwa na mtafiti kwa kuzingatia sifa na tabia zao ambazo zinaweza kukidhi kuwakilisha kundi kubwa la watu au vitu linalotarajiwa kutafitiwa. Katika utafiti huu, mtafiti alikusanya semi105na hatimae kuteua semi 52 kama sehemu ya sampuli ya utafiti huu. Mtafiti amechagua sampuli hii akiamini kuwa idadi ya hiyo ya semi ambazo zinapatikana katika kuta za nyumba hizo zitaweza kujibu maswali ya utafiti huu.

#### 3.4.2 Usampulishaji

Usampulishajini kitendo cha kuchaguwa au kupata kikundi fulani ili kuwakilisha kundi lengwa. Kothari (2014) anaifafanua dhana ya usampulishaji kwamba

nimchakato ambao humuwezesha mtafiti kuchagua wateuliwa ambao anaamini watampatia data zitazojibu maswali ya utafiti wake. Hivyo, katika utafiti huu, mtafiti alitumia usampulishaji lengwa. Usampulishaji lengwa ni aina ya usampulishaji ambao mtafiti huenda moja kwa moja katika chanzo cha taarifa akiamini kuwa atapata data alizozikusudia (Babbie, 1999). Usampulishaji lengwa ni muhimu katika kutoa data za uhakika na kuokoa muda. Hivyo, katika utafiti huu mtafiti alituumia uteuzi lengwa ambapo alizikusanya semi 105 na baadae kuchagu semi 52 kati ya semi hizo.

## 3.5 Aina ya Data Zilizokusanywa

Katika utafiti huu mtafiti alikukusanya data za msingi ambazo zilipatikana katika semi zilizochorwa kwenye kuta za nyumba za vijiji za Pemba. Ufafanuzi wa aina hii ya data ambazo zilikusanywa na mtafiti ni kama ifuatavyo:

### 3.5.1 Data za Msingi

Data za msingi ni zile zinazokusanywa kwa mara ya kwanza na hivyo ni data halisi (Kothari, 2014). Data hizi za msingi huwa hazijapata kukusanywa na mtafiti mwingine kwa ajili ya utafiti kama huu ambao unakusudiwa kufanywa. Data za msingi katika utafiti huu zilikusanywa kutoka katika semi zinazoandikwa kwenye kuta za nyumba za vijiji Pemba.Data hizo ndizo ambazo zilifanyiwa uwasilishaji na uchambuzi katika sura ya nne ya tasnifu hii.

## 3.6 Njia za Kukusanya Data

Ukusanyaji wa data ndio hatua muhimu katika utafiti wa kisayansi. Kothari (2014) anafafanua dhana ya ukusanyaji wa data kama zoezi la awali katika utafiti ambalo

humuwezesha mtafiti kupata taarifa alizozikusudia ili kumfikisha katika madhumuni yake ya utafiti. Aidha, Kothari anasisitiza kuwa hatua ya uwasilishaji na uchambuzi wa data haiwezi kufanyika kabla ya hatua hii ya ukushanyaji wa data. Katika utafiti huu,data zilikusanywa kwa kutumia njia ya usomaji makini na njia ya ushuhudiaji.

### 3.6.1 Njia ya Maktabani

Njia hii imetumika kukusanya data za upili. Kothari (2004)anaeleza kuwa njia ya maktabani ni njia ya ukusanyaji wa data ambapo mtafiti husoma machapisho mbalimbali na kudondoa data anazozikusudia. Katika utafiti huu, data zilizokusanywa kwa kutumia njia ya maktabani ni data za upili.

### 3.6.2 Njia ya Maskanini

Njia ya maskanini ni ile njia inayotumiwa na mtafiti kufika katika sehemu (eneo) husika ambapo watafitiwa wake watapatikana, kama vile mitaani au shuleni (Kothari, 2014). Katika utafiti huu data za msingi zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya ushuhudiaji. Mbinu hii imefanyiwa ufafanuzikama ifuatavyo:

#### (i) Mbinu ya Ushuhudiaji

Kothari (2014) anaelezakwamba hii ni mbinu ya ukusanyaji wa data za msingi ambapo mtafiti huenda moja kwa moja kwenye chanzo cha data anazozihitaji. Ili kuzipata data za utafiti huu, mtafiti alikwenda moja kwa moja kwenye nyumba za vijiji ambapo kuna maandishi katika nyumba hizo. Kisha alizinukuu semi hizo katika shajara. Baada ya kuzinukuu data hizo mtafiti alizipitia kwa umakini ili kudondoa data zilizojibu maswali ya utafiti huu.

### 3.7 Usahihi, Kuaminika kwa Data na Maadili ya Utafiti

Sehemu hii inafafanua vipengele vya usahihi wa data, kuaminika kwa data na maadili ya utafiti namna yalivyozingatiwa tangu mwanzo wa utafiti huu hadi kukamilika.

#### 3.7.1 Usahihi wa Data

Usahihi wa mbinu za kukusanyia data ni utaratibu unaowezesha kupatikana kwa data sahihi na za kuaminika za utafiti (Cohen na wenzake, 2000). Usahihi wa data katika utafiti huu ulihakikishwa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini na upitiaji wa nyaraka. Katika uchambuzi wa data, mkabala wa kimaelezo ndio uliotumika. Usahihi wa mbinu hizi unatokana na ukweli kuwa upungufu wa kila moja unakamilishwa na ubora wa mbinu nyengine. Vile vile, usahihi wa mbinu na nadharia za uhakiki wa fasihi zilizotumika katika utafiti huu zilijadiliwa baina ya mtafiti na msimamizi.

#### 3.7.2 Kuaminika kwa Data za Utafiti

Kuaminika kwa data za utafiti kunatokana na uwezo wa mbinu za utafiti kutoa matokeo yale yale ya utafiti unaporudiwa kwa kutumia mbinu zile zile (Kothari, 2014). Kuaminika kwa data kunajitokeza pale ambapo kunakuwa na uhusiano ama mlingano wa taarifa zinazotolewa na watu wale wale kwa muda tofauti (Furlong na Lavelace, 2000). Katika utafiti huu kuaminika kwa data kulihakikishwa kwa kutumia nadharia ya Simiotiki na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji.

#### 3.7.3 Maadili ya Utafiti

Maadili ya utafiti huhusishwa na mila na desturi ambazo jamii huziamini katika eneo ambalo mtafiti analenga kuchunguza kitu au jambo fulani. Lengo la maadili katika

utafiti ni kulinda masuala ya kibinaadamu yanayoaminiwa na jamii. Pia, kuhakikisha kuwa utafiti unafanyika katika muktadha unaokubalika; kwa mtu mmoja mmoja, kikundi cha watu au jamii kwa ujumla na kuhakikisha kuwa miradi ya kitafiti inazingatia maadili, kama vile; ukusanyaji wa data kwa usahihi, utunzaji siri na utoaji wa habari,

Hivyo, katika utafiti huu maadili ya utafiti yalizingatiwa ipasavyo kabla na baada ya kukusanya data. Kwasababu utafiti huu ulikuwa wa uwandani mtafiti alihakikisha kuwa data kutoka katika vyanzo vya taarifa zimenukuliwa na kupangwa kwa umakini mkubwa.

## 3.8 Hitimisho

Sura hii imeelezea mbinu za utafiti ambazo mtafiti alizitumia katika utafiti wake. Sura hii imewasilisha mbinu hizo ambazo ni eneo la utafiti, usanifu wa utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, aina za data, ukusanyaji wa data na mwisho sehemu hii inaelezea usahihi wa data, kuaminika kwa data na maadili ya utafiti. Kwa ujumla katika sehemu hii mtafiti ameonesha namna data alivyozipata na hatimae kufikia hitimisho la utafiti huu. Sura inayofuata inahusu uwasilishaji na uchambuzi wa data za utafi.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI

## 4.0 Utangulizi

Sura hii inahusu uwasilishaji na uchambuzi wa data za utafiti kwa madhumuni ya kukamilisha malengo ya utafiti huu. Uwasilishaji na uchambuzi wa data za utafiti umefanywa kwa kuzingatia malengo mahususi. Hivyo basi, sura hii imegawika katika sehemu ndogo ndogo tatu ambazo ni kwanza, imebainisha semi zinazoandikwa katika kuta za nyumba za vijiji za Pemba, pili kubainisha matumizi ya lugha katika semi hizo na sehemu ya tatu inatathmini dhamira zinazopatikana katika semi zinazoandikwakwenye kuta za nyumba za vijiji za Pemba. Hivyo data za utafiti huu zimewasilishwa na kufanyiwa uchambuzi kama ifuatavyo:

## 4.1 Semi Zinazoandikwa katika Kuta za Nyumba za Vijiji Kisiwani Pemba

Lengo mahususi la kwanza la utafiti huu lilikuwani kubainisha semi zinazoandikwa katika kuta za nyumba za vijiji Kisiwani Pemba. Ili kulifkia lengo hili mtafiti alizitalii data za utafiti huu na kuzibainisha semi hizo kutegemea miktadha ya matumizi. Katika kuzibainisha semi hizo mtafiti alibaini kuwa zipo semi zilizochorwa katika kuta za nyumba Kisiwani Pemba ambazo zimekuwa zikitumika ili kusawiri miktadha tofauti. Kwa hivyo, semi hizo ziliweza kubainishwa huku baadhi zikiingia katika kategoria zaidi ya moja kutokana na matumizi changamano ya matumizi yake katika jamii. Kwa mfano, semi inayosema “Maisha siri” inaingia katikika kategoria ya semi zinazoelezea utamaduni wa jamii ya Pemba na Uswahilini kwa ujumla ambapo jamii hiyo haipaswi kueleza hadharani kila jambo linalohusu maisha yake. Kwa upande mwengine, semi hii inatumika katika muktadha

wabiashara ili kutia mkazo watu kufanya bidii katika kazi kwani biashara ina siri kubwa katika mafanikio. Hivyo basi, semi hizo zinaweza kubainishwa kama ifuatavyo:

### 4.1.1 Semi Zinazoonesha Utabaka

Kutokana na utafiti uliofanyika, mtafiti amebaini kuwa tapo la kwanza la semi zilizochorwa katika kuta za nyumba za vijiji za Pemba ni zile ambazo huonesha matabaka yaliomo katika jamii hiyo. Mfano wa semi hiyo ni ule unaosema `Mbwa kachoka.` Msemo huu hutumiwa na jamii ili kuonesha namna jamii ilivyogawika kitabaka. Picha tunayoipata kupitia msemo huu ni kwamba tabaka la chini ambalo linawakilishwa na ishara ya `mbwa` kuwa limechoka kutokana na ukandamizaji.

Vile vile, methali isemayo “aliyejuu mngoje chini” inaonesha namna jamii ilivyo na utabaka kutokana na vyeo. Kutokana na methali hii jamii inaonyesha kuwa cheo ni nafasi ya muda. Vyovyote iwavyo, ipo siku yule aliye juu atakuwa katika tabaka la chini na hivyo kubakia akijuta kutokana na yale aliyolitendea tabaka la chini.

Pia semi inayosema “Zimwi likujualo halikuli likakwisha” unaonesha namna ndugu na jamaa walivyo na msaada mkubwa katika maisha ya kila siku. Tunachokibaini kupitia semi hizi ni taswira ya mawazo ya Karl Marx (1977) yanayoeleza kwamba utabaka ulijikita katika mifumo ya uzalishaji mali ambayo iliendelezwa na tabaka la juu. Naye Wafula (1997) anaeleza kuwa fikra ya utabaka haipatikani katika watu wa kabila au rangi moja tu; bali inapatikana katika kizazi chochote cha mtu ambapo mazingira yatatokezea yanachochea kuchipuka na kushamiri kwake. Hii ni kusema

kuwa hata jamii ya Wapemba nayo inakabiliwa na tatizo la utabaka kutokana na kile kinachojidhihirisha katika semi hizo.

### 4.1.2 Semi za Umoja na Mshikamano

Data zinaonesha kuwa zipo semi katika kuta za nyumba za vijiji za Pemba ambazo zinalenga kujenga umoja na mshikamano katika jamii. Mifano ya semi hizo ni ule usemao "Umoja ni nguvu," ambao umechorwa katika ukuta wa nyumba yenye kutumiwa na timu ya Umoja ni Nguvu inayopatikana katika kijiji cha Kiungoni Wilaya ya Wete Pemba. Mfano mwengine wa semi wenye kuingia katika kategoria hii ni ule unaosema "Penye wengi pana mengi" ambao unahamasiha umoja namshikamano miongoni mwa wanajami.

### 4.1.3 Semi za Imani

Tapo jengine la semi zilizoandikwa katika kuta za nyumba za vijiji Kisiwani Pemba ni semi zinazosawiri masuala ya imani. Moja ya semi hizo ni ile isemayo "Mungu atosha." Katika semi hii tunaibuliwa imani ya kwamba Mungu ndie mwenye uwezo wa kumtosheleza mtu juu ya kila kitu. Kihistoria semi hii hutumiwa na wanajamii ambao wanaamini Mwenyezi Mungu mmoja kama ilivyo kwa wanajamii wa Kisiwa cha Pemba.

Msemo mwengine ambao mtafiti alibaini umechorwa katika kuta za nyumba za vijiji za Pemba ambao unasawiri suala la imani ni ule usemao "Mungu mkubwa." Msemo huo unaonesha uwezo wa Mungu. Aidha, msemo wa "Mungu atosha" ni miongoni mwa semi zinazoakisi masuala ya imani miongoni mwa wanajamii. Wenye kuamini

kuwepo kwa Mungu wana imani kuwa Mungu ndiye wa kutegemewa na ndiye mwenye kuweza kutatua shida za watu.

Kwa ujumla tunaporejelea nadharia ya Mwitiko wa Msomaji kama nadharia hiyo inavyoelezwa na Wafula (2007) mtafiti anapata fursa ya kuziweka semi hizo katika kundi la semi zinazojadili suala la imani kuhusu uwezo wa Mungu ama uhusiano uliopo kati ya mtu na Mungu. Matokeo haya yanaonesha kuwa imani ni moja kati ya suala linalojibainisha miongoni mwa wanajamii wa jamii husika.

### 4.1.4 Semi za Kuhamasisha Kazi

Aina nyengine ya semi zinazoandikwa katika kuta za nyumba za vijiji za Pemba ni zile zinazohamasisha kazi. Semi hizo huwa na dhima ya kuonesha umuhimu wa kufanya kazi ili kujenga jamii mpya endeleviu. Mfano wa semi hizo ni methali inayosema "Mtaka cha mvunguni sharti ainame." Methali hii inadokeza namna wanajamii wanavyopaswa kufanyua kazi ili kufikia malengo waliyojiwekea.

Msemo mwengine ambao huweza kuekwa katika mfano wa methali zinazojadili suala la kazi ni pamoja na methali inayosema "Ukiona vyaelea ujue vimeundwa." Msemaji anaposema ukiona vyaelea ana maana ya kwamba tunapoona mafanikio na \`vimeundwa\` ana maana ya kwamba mtu alifanya juhudi katika kazi hadi kufikia hatua hiyo ya mafanikio.

Vile vile, data zinaonyesha kuwa katika baadhi ya kuta za nyumba za vijiji za Pemba kuna msemo unaoeleza "Lamnyonge halendi joshi," ambao umetumika katika miktadha ya kufanya kazi. Semi hizo hutumiwa katika miktadha ya kazi ili

kutekeleza jukumu muhimu kama mwanajamii. Mawazo haya yanashadidiwa na Jesse (2018) anapoeleza kwamba kazi ni kipengele kimoja cha kijamii. Anaendelea kueleza kwamba mifumo ya kiuchumi hufungamana na elimu na kazi. Kuhusu kazi wale wenye kipato cha chini hujikuta wakifanya kazi za watu wa hadhi ya chini na wale wenye kipato kikubwa hujikuta wakifanya kazi za watu wenye hadhi ya juu. Huo ndio mtindo wa maisha katika jamii yoyote.

### 4.1.5 Semi Zinazokosoa

Moja kati ya kazi ya fasihi ni kuikosoa jamii katika vipengele mbalimbali vya maisha (Mulokozi, 1996). Hivyo data zilizokusanywa na mtafiti zinaonesha kuwa katika kuta za nyumba za vijiji za Pemba kuna semi zilizochorwa ambazo zinaweza kubainishwa na kuekwa katika tapo hili. Mifano ya semi zenye kusawiri dhima hii ni pamoja na methali inayosema "Nilijua roho zitawauma." Kupitia msemo huu watu wanakosolewa kutokana na tabia ya chuki na choyo.

Mfano mwengine wa semi inayopatikana katika kuta za nyumba za vijiji za Pemba wenye kuingia katika kategoria hii ya semi ni ule unaosem "Usilolijua litakusumbua." Katika msemo huo wanajamii wanakosolewa kufanya maamuzi kuhusu jambo lolote wasilolijua kwani huweza kufikia maamuzi yasiyo sahihi. Hivyo ipo haja ya kufanya uchunguzi kuhusu maamuzi yanayofanyika ili kuepukas kukosea kwenye maamuzi hayo.

Vile vile, semi inayosema "Usijaze masusu kwa mambo yasiyokuhusu" wanakosolewa wanajamii wenye tabia ya kujiingiza katika kila jambo ambalo kamwe haliwahusu. Picha ya `kujaza masusu` inayojengwa katika semi hii inamaana

ya tabia ya baadhi ya watu kuchukua maneno kutoka kwa mtu au kundi la watu na kuyapeleka kwa mtu au watu wengine kwa nia ya kuwagombanisha. Hivyo wenye tabia hiyo wanatakiwa kuacha mara moja.

Aidha, msemo unaosema "Sema nao, cheka nao, kusema ndio kazi yao" ni msemo unaotumiwa na wanajamii ili kukosoa baadhi ya wanajamii kuhusu suala la kusengenya. Pia, msemo unaosema "Munajenga nyumba zenu hamuzitii penu, mutasema wapi vichakaa vyenu?" unalenga kufichua tabia mbaya za baadhi yawatuwenye tabia ya kuwasema wengine. Mwisho msemo unaosema "Kila waonalo wasema na hili kaseme" huu ni msemo ambao kwa muda mkubwa umekuwa ukionekana umeandikwa katika vazi la kanga lakini kwa sasa unajitokeza hata katika kuta za nyumba ili kuikosoa jamii kutokana na tabia ya baadhi ya watu kusema kila kitu wanachokiona.

Kwa kutumia nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ni kwamba semi zilizochorwa katika kuta za nyumba zinaingia katika tapo la methali zenye kuikosoa jamii. Kwani jamii ya Wapemba kama zilivyo jamii nyengine ulimwenguni imekuwa ikifanya matendo yanayokubalika na yale yasiyokubalika na wanajamii hao. Ili kuyakosoa matendo hayo watu hutumia maandishi ya kwenye kuta za nyumba ili kutoa hisia zao kuhusu mambo mbali mbali.

### 4.1.6 Semi Zenye Kukejeli

Vile vile, data zilizokusanywa na mtafiti zinaonesha kuwa zipo baadhi ya semi zinazoandikwa kwenye kuta za nyumba za vijiji za Pemba ambazo zinaweza kuekwa kwenye kategoria ya semi zenye dhima ya kukejeli baadhi ya matendo ya wanajamii.

Mifano ya semi hizo ni "Utajiju," ambao hutumika kumkejeli mtu aliyefanya jambo bila ya kuzingatia athari zake na hatimae akapata matarajio hasi. Pia, semi inayosema "bure mnajipa dhiki," inatumika kuwakejeli watu ambao hushughulikia jambo ambalo hawawezi kulifanya liathirike.

Semi nyengine inayoingia katika kundi hili ni ile inayosema "Bora adui shetani kama adui kiumbe." Semi hii inamkejeli mtu mwenye tabia ya uadui na kulinganishwa na shetani ambapo mtu huyo anaonyeshwa kuwa huwa ni mbaya kuliko hata huyo shetani. na semi inayosema "Bure munajipa dhiki kujikwaa na vizingiti linalowakera ni lipi" inalengo la kuwakejeli wenye tabia ya kuchunguza mienendo ya watu wengine kwa muelekeo hasi.

Tunapochunguza matendo yasiyokubalika ndani ya jamii na namna yanavyokejeliwa kwa kutumia fani ya semi zinazopatikana katika kuta za nyumba za vijiji za Pemba kunapatikana picha ya maisha ya wanajamii hao ambayo ni kwamba baadhi ya matendo ya wanajamii si yenye kukubalika. Kwa kutumia nadharia ya Mwitiko wa Msoamaji inayompatia fursa mhakiki wa kazi ya fasihi kuihukumu kazi ya fasihi anayoisoma kutekegemea na tajriba ya jamii ni kwamba mifano ya semi zilizobainishwa katika kundi hili hutumika kama kioo cha kuikejeli jamii na kuirekebisha.

### 4.1.7 Semi za Utamaduni

Khamis (2016) anaeleza kuwa dhana ya utamaduni ni jumla ya maisha ya watu katika jamii au jumuia zao katika hali ya kutumia mawazo na vitu katika mazingira yao. Maisha hayo yanajumuisha vipengele vy utamaduni kama mila, silka, desturi,

imani, itikadi na jadi za watu katika mazingira yao mahususi ya nchi yao. Anaendelea kueleza kwamba pamoja na ujumla huo wa utamaduni katika nchi moja kunajitokeza tofauti ndogo ndogo za utamaduni kati ya mkoa na wilaya au kijiji na kijiji.

Moja kati ya semi inayoingia katika kundi hili ni ule unaosema "Piga hodi mara tatu" ambao huwa unachorwa katika kuta za nyumba karibu na mlango wa kuingilia katika nyumba za vijiji za Pemba. Semi hii inaonyesha utamaduni wa jamii hiyo ambao hauruhusu mtu asiyeishi katika nyumba husika kuingia ndani bila ya kupiga hodi mara tatu ili kupata ruhusa ya kuingia. Aidha, semi isemayo "Maisha siri" ni mfano mwengine wa semi zinazoandikwa katika kuta za nyumba za vijiji za Pemba ambao unaingia katika semi za utamaduni kwani jamii hii inaamini kuwa maisha ni siri ya mtu binafsi, kuhusu kupata au kukosa hakuna haja ya kusimulia watu wengine.

Semi nyengine ambazo zinaingia katika kategoria hii ya semi za utamaduni ni pamoja na "Usimnunie sisimizi sukari haimalizi" na "Ukijali tutakujali usipotujali potelea mbali." Kwa ujumla mtafiti anaporejelea nadharia ya Mwitiko wa Msomaji anapata kauli ya kueleza kuwa semi hizo zinatoa picha halisi ya maisha ya jamii ya Wapemba kuhusu kipengele cha utamaduni wa jamii hiyo.

### 4.1.8 Semi za Mapenzi

Mapenzi ni hisia nzito ya moyoni inayomfanya mtu avutiwe, athamini na ajali mtu, kitu au jambo (BAKIZA, 2010). Data zinaonesha kuwa katika kuta za nyumba za vijiji za Pemba kuna semi ambazo zinasawiri miktadha ya mapenzi. Kwa mfano, usemi unaosema "I love you," ambao uko katika lugha ya Kiengereza wenye maana

ya `Nakupenda` hutumika kuonyesha hisia za mapenzi kati ya mwanamke na mwanamme. Pia, semi inayosema “Tulia tuishi wazuri haweshi” ni mfano mwengine wa semi inayopatikana katika kuta za nyumba za vijiji Kisiwani Pemba. Usemi huu unatupatia picha ya hisia za mwanamke ambaye analengo la kumnasihi muume wake atulize mapenzi yake kwake kwani wazuri katika jamii ni wengi.

Semi nyengine zinazoingia katika kundi hili la semi za mapenzi ni “Nina weye tu.” Mapenzi yanayosawiriwa hapa ni yale ya kutoa ithibati kwamba hakuna mwengine katika penzi hilo. Aidha, semi isemayo “Wazuri haweshi” inajidhihirisha katika kuta za nyumba za vijiji za Pembakwa lengo la kuhamasisha mapenzikati ya wanandoa.

Mwisho, semi inayosema `Nimekichomeka kisu na mpini hata mukisema iwe nini?` ni miongoni mwa semi zinazoandikwa katika kuta za nyumba za vijiji za Pemba ili kuonesha kuwa mapenzi ya dhati hayawezi kutenganishwa. Semi hizi ni sehemu ya kipengele cha jamii ambacho kinaakisiwa katika jamii. Ukweli ni kwamba hatuwezi kutenganisha mapenzi na jamii kwa sababu ni kipegele kinachoashiria utamaduni wa jamii husika kama aelezavyo Althusser katika Jessee (2018) kwamba mapenzi ni moja ya kigezo cha utamaduni.

### 4.1.9 Semi Zinazoifunza Jamii

Moja kati ya kazi kuu za fasihi ni kutoa mafunzo katika jamii (Mulokozi, 1996). Hivyo basi, data zilizokusanywa na mtafiti zinaonesha kwamba katika kuta za nyumba za vijiji za Pemba zipo semi zinazoweza kuekwa katika kundi la semi zinazoifunza jamii. Semi hizo ni kama zifuatazo:

Usimuogope mbwa mwenye meno, muogope jirani mwenye maneno
Ukimnunia jirani uombe chumvi kwa nani?
Waache waseme
Pita na zako
Usijaze masusu kwa mambo yasiyokuhusu
Mbaya halisi na wema hakosi
Usilolijua litakusumbua
Wema hauna cheti na ubaya hauna krediti
Ukiona macho yanalia ujue moyo umezidi kuvumilia

Katika semi hizo tunabaini kwamba tunapata mafunzo tofauti katika miktadha ya maisha ya kila siku. Kwa mfano, semi "Ukimnunia jirani uombe chumvi kwa nani?" ni semi ambayo inatoa mafunzo kuhusu umuhimu wa kuishi vizuri na majirani. Vile vile, katika miktadha ya maisha ya ujirani kunatumiwa semi isemayo "Usimuogope mbwa mwenye meno, muogope jirani mwenye maneno." Kupitia semi hii inatufundisha namna jirani anapogeuka kuwa sawa na adui kutokana na kutumia maneno vibaya.

Kwa kutumia nadharia ya Mwitiko wa Msomaji mtafiti amebaini kuwa semi zilizobainsihwa katika sehemu hii zimeakisi mafunzo katika miktadha ya maisha ya wanajamii. Hali hii ndiyo inayoelezwa na Njogu na Chimerah (1999) kwamba fasihi na mwanafasihi ni vitu viwili ambavyo haviwezi kujitenga na matukio ya jamii husika. Hii inatokana na ukweli kwamba wanajamii hujifunza kupitia tanzu mbalimbali za fasihi.

### 4.1.10 Semi Zinazoonyesha Utabaka

Utabaka ni makundi ya watu yaliyomo katika jamii. Makundi hayo huweza kuwa yanatokana na tofauti ya kipato, elimu ama ujinsia (Jilala, 2016). Data

zilizokusanywa na mtafiti zinaonesha kuwa katika kuta za nyumba za vijiji za Pemba kuna semi ambazo mtafiti anaweza kuziweka katika tapo la semi zinazosawiri utabaka katika jamii. Miongoni mwa semi hizo ni kama hizi zifuatazo:

Mbwa kachoka
Aliye juu mngoje chini
Zimwi likujualo halikuli likakwisha
Sisi ni jabali, changarawe hazitujali
Mchawi house
Nyumba ya bilisi
Nasi huku
Si gogo wala si shina, matawi ndio fitina.

Katika semi za hapo juu tunapozichunguza ni wazi kwamba tunaweza kugundua namna zinavyosawiri suala la utabaka. Kwa mfano, "Nasi huku" unadhima ya kuonesha namna tabaka la mtumiaji wa semi hiyo linavyotoa kilio ili kupata haki. Aidha, kwa kutumia semi "Zimwi likujualo halikuli likakwisha" tunapata picha ya utabaka unaoendelezwa kutokana na upendeleo unaotokana na watu kujuana. Vile vile, semi inayosema "Sisi ni jabali changarawe hazitujali" inaonyesha namna tabaka lenye nguvu linavyoendeleza ukandamizaji dhidi ya tabaka la chi kutokana na nguvu lilizonazo.

Sula la utabaka kama linavyodhihirika katika semi hizi linaonesha kuwa ni picha inayotupatia taswira ya maisha ya jamii ya Wapemba ambao kama zilivyo jamii nyingi ulimwenguni imekabiliwa na suala la utabaka. Kwa ujumla kwa kutumia nadharia ya Mwitiko wa Msomaji mtafiti anaweza kuhitimisha kuhusu suala la semi zilizochorwa katika kuta za nyumba za vijiji za Pemba kwa kueleza kuwa semi hizo zinaibua na kukemea suala hili la utabaka.

## 4.2 Lugha katika Misemo Iliyoandikewa kwenye Kuta za Nyumba za Vijiji za Pemba

Lengo mahususi la pili la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza matumizi ya lugha namna yanavyojitokeza katika semi zilizochorwa kwenye kuta za nyumba za vijiji za Pemba. Baada ya mtafiti kuzikusanya data zinazohusu semi hizo, alizitalii na kubaini kuwa semi hizo zinatumia vipengele kadhaa vya lugha. Hivyo basi, katika sehemu hii mtafiti alifanya uwasilishaji na uchambuzi wa data zinazohusu matumizi ya lugha kama yanavyojitokeza katika semi hizo.

### 4.2.1 Matumizi ya Lahaja

Lahaja ni tofauti ya matumizi ya vipengele vya lugha katika lugha moja. Data zilizokusanywa na mtafiti zinaonesha kuwa semi zilizochorwa katika kuta za nyumba za vijiji huko kisiwani Pemba zina matumizi ya lahaja ya Kipemba. Matumizi haya ya lahaja yanajidhihirisha kutokana na uteuzi wa maneno ambayo yanapatikana miongoni mwa watumiaji wa lahaja hiyo. Mathalani katika msemo unaosema "Kila uonalo wasema na hili kaseme" kuna matumizi neon la kilahaja ambalo ni "uonalo" ambalo katika lahaja ya Kiswahili sanifu ni "unaloliona."

Vile vile, kuna matumizi ya lahaja katika methali inayosema "Usijaze masusu kwa mambo yasokuhusu." Katika dondoo hilo, data zinaonesha kuwa kuna matumizi ya neno "masusu" ambalo lina maana ya "tenga ambalo hutumika kuingiza matunda kama vile maembe, ndizi, chungwa nakadhalika ili kusafirishwa kutoka eneo moja na jengine." Katika msemo huu, neno "masusu" limetumika ili kukamilisha muundo wa kishairi. Kama asemavyo Mulokozi (1996) baadhi ya methali huwa na muundo wa kishairi.

Athari za lahaja ya Kipemba pia zinajitokeza katika msemo unaosema “Katie chomwe.” Neno “chomwe” kama linavyojidhihirisha katika msemo huu, katika lahaja ya Kiswahili sanifu lina maana ya “Chumvi ya mawe.” Msemo huu una maana ya kuzidisha jambo ambalo umeliona ama kulisikia kwa lengo la kufarakanisha ama kujifaidisha kwa malengo ya mzungumzaji binafsi. Aidha, data zinabainisha kuwa semi ziandikwazo katika nyumba hizo zina athari za uteuzi wa maneno yenye maumbo ya lahaja ya Kipemba jambo ambalo huweza kutambulisha watumiaji wa semi hizo.

Watu wanaoandika semi za kwenye kuta za nyumba huamua kutumia lahaja ya Kipemba kutegemea miktadha ya ujumbe wanaouzungumzia. Hii ni kwa sababu uteuzi wa matumizi ya lugha huwa unategemea miktadha husika. Kama mawazo haya yanavyothibitishwa na Mlaga (2017) kuwa uteuzi wa matumizi ya maneno miongoni mwa wahusika hutegemea miktadha. Kutokana na msingi huo miktadha ya matumizi ya maneno ya lahaja katika semi zilizotafitiwa zinalenga kuisawiri jamii husika.

### 4.2.2 Balagha

Balagha ni matumizi ya lugha yaliyokiuka uhalisia wa jambo linaloelezewa. Ndungo na Wafula (1993) wanasema kuwa matumizi haya ya lugha ni kutia chumvi. Data zilizokusanywa na mtafiti zinaonesha semi zilizoandikwa kwenye nyumba za vijiji za Pemba zinatumia mbinu ya matumizi ya lugha ya balagha. Kwa mfano, msemo unaosema “Sisi ni jabali, changarawe hazitujali” kuna matumizi ya mubalagha kutokana na mwandishi wa semi hiyo kujifananisha na jabali na kuwadogesha wengine akiwafananisha na “changarawe.”

Katika semi hiyo, matumizi ya balagha yanasawiri nadharia ya Simiotiki kwenye Msimbo wa Kiishara ambao unaona kuwa fasihi hutumia viashiria mbalimbali ambavyo vinatumiwa na wanajamii. Ishara ya "jabali" kama inavyotumika katika semi hii ni kiwakilishi cha kutotetereka na kuwa na umakini wa hali ya juu. Kwa upande mwengine neon "changarawe" kama linavyotumika katika semi hii ni ishara inayoonyesha "udhaifu na kutokuwa imara juu ya jambo fulani."

Mfano mwengine wa matumizi ya lugha ya balagha katika semi za kwenye kuta za nyumba za vijji za Pemba ni ule unaosema "Nimekichomeka kisu na mpini hata mkisema ndio iwe nini?" Katika semi hiyo tunaelezwa namna matumizi ya chuku yanavyojidhihirisha kutokana na mwandishi kueleza kuwa amekichomeka kisu na mpini, na hata watu wakisema hakuna lolote litakalokuwa. Kauli hiyo ni chuku kutokana na ukweli kwamba kisu ni kifaa hatari na kinapomchoma mtu huleta matatizo. Aidha, katika hali ya kawaida mtu hawezi kukichomeka kisu pamoja na mpini wake bila ya mtendwa kujali.

Kwa ujumla matumizi ya lugha ya chuku katika semi zilizoandikwa kwenye nyumba za vijiji za Pemba yanatumika ili kuonyesha ukengeushi wa kuelezea jambo linaloelezwa kutokana na uhalisia wake katika jamii. Mawazo haya yanaakisi mtazamo wa Ndungo na Wafula (1993) kwamba maneno katika lugha ya chuku huwa yamechaguliwa kwa uangalifu ili kuibua hisia yasisitize jambo. Mawazo haya yanaakisi msimbo wa kiseme unaopatikana kwenye nadharia ya Simiotiki ambao unahusiana na jinsi matumizi ya ishara yanavyotumika kuisawiri jamii.

### 4.2.3 Kejeli

Hii ni mbinu ambayo humdunisha mtu. Ndungo na Wafula (1993) wanaeleza kuwa kejeli ni matumizi ya lugha kwa lengo la kumdharau, kumchekelea au kumfanyia mzaha mtu. Data zilizokusanywa zinaonesha kuwa semi zilizoandikwa kwenye nyumba za vijiji za Pemba zinatumia lugha ya kejeli. Kwa mfano, kuna msemo unaosema "Nyumba ya bilisi." Msemo huu umeandikwa ili kudhihaki baadhi ya watu waliomo katika jamii.

Semi nyengine ambayo inasawiri matumizi ya kejeli ni ule unaosema "Bora adui shetani kama adui kiumbe." Kauli hii inalenga kukejeli watu ambao wanafanya uadui dhidi ya wengine. Katika usemi huo jamii inatakiwa kuondokana na tabia hiyo ya uadui kwani ni kitendo kibaya kuliko hata uadui anaoufanya bilisi.

### 4.2.4 Tashihisi

Senkoro (1982) anfasili kuwa tashihisi ni tamathali ya usemi ambayo wakati mwingine huitwa tamathali ya binadamu kutokana na kukipa kitu au dhana fulani sifa za binadamu. Data zilizokusanywa na mtafiti zimeonyesha kwamba semi zilizoandikwa katika nyumba za vijiji za Pemba pia zimekuwa zikitumia kipengele hiki cha lugha. Kwa mfano, semi inayosema "Si gogo wala shina matawi ndio fitina." Katika semi hii matawi yanapewa uwezo wa binadamu wa kufanya fitina jambo ambalo haliwezi kutendwa na kiumbe kisicho na sifa ya binadamu kama vile matawi ya mjiti.

Vile vile, "Ukiona macho yanalia ujuwe moyo umezidi kuvumilia."Katika dondoo hilo macho yamepewa sifa ya matendo ya binadamu ya kulia. Aidha, katika usemi

huo, “moyo” ambao ni kiungo cha mwili kinapewa uwezo wa binadamu wa kuchoka kuvumilia. Misemo mingi imekuwa ikitumia mbinu hii ya tashihisi ambapo kiungo, mnyama, mjiti ama sehemu ya mjiti hutumika kujenga tashihisi ndani yake.

Kwa kutumia nadharia ya Simiotiki, msimbo wa kiishara wa nadharia hiyo unatubainishia namna semi zinazoandikwa katika nyumba za vijiji za Pemba zinavyotumia kipengele hiki cha tashihisi katika kujenga usanii. Vitu hupewa uwezo wa binadamu ili kujadili masuala muhimu yanayoihusu jamii hiyo.

### 4.2.5 Misemo

Dhana ya misemo inarejelea kifungu kifupi cha maneno kinachobeba maana kimafumbo ambayo imekusudiwa kutoa funzo kwa jamii. Pia, huelezwa kuwani utumiaji wa maneno yanayotumika mara kwa mara kama yalivyo katika mazingira maalumu ambayo huleta maana maalumu (Senkoro, 2011). Data zilizokusanywa na mtafiti zimeonyesha kuwakatika vijiji za Pemba kuna matumizi ya misemo ambayo huchota ujumbe uliokusudiwa na wanajamii husika. Kwa mfano, *Bora adui shetani kama adui kiumbe*. Msemo huo unatumiwa kukejeli baadhi ya tabia za wanajamii zisizokubalika. Aidha, msemo usemao *Maisha siri* unadokeza miiko kuhusu maisha ya wanajamii kuhusu ukweli wa maisha ya kila siku kutokana na tofauti ya kipato.

Vile vile, msemo unaosema *Sema nao, cheka nao kusema ndio kazi yao*ni msemo ambao umeandikwa katika kuta za nyumba za vijiji za Pemba ili kukosoa tabia za kusengenya. Tabia hiyo imekuwa ikifanywa na watu ambao tunaishi nao katika maisha ya kila siku. Mawazo hayo yanajitokeza pia katika msemo unaosema *Kikulacho ki nguoni mwako* ambao unalengo la kufichua watu wa karibu ambao wanakuwa wasaliti na kutekeleza uadui kwa ndugu ama jamaa.

Mtafiti anapoitalii misemo inayoandikwa katika nyumba za vijiji za Pemba amebaini kuwa nyumba hizo zinaandikwa misemo inayolandana nanadharia ya Simiotiki kwenye msimbo wa Kiurejelezi ambao kwa mujibu wa Barthes (1994) unajengwa kutokana na viashiria vya utamaduni unaorejelewa katika ngazi inayohusika ya fasihi. Wamitila (2002) anaeleza kuwa urejelezi huo huunda uhalisi mahususi na matumizi ya vitu fulani vinavyoeleweka na wasomaji na kwa njia hiyo huipa kazi fulani ya nguzo ya kiutamaduni. Kutokana na msingi huo, semi hizo zimechotwa katika jamii kama sehemu ya kuimwirika jamii na kuipa maelekezo.

### 4.2.6 Methali

Methali ni usemi mfupi wenye maana pana, busara na hekima ambao unakusudiwa kusema jambo maalumu lakini kwa kufumba. Mulokozi (1996), Wamitila (2001) na Mbonde (2005)wanamawazo yanayofanana kuhusu dhana ya methali ambapo wanaeleza kuwa methali huwa ni usemi mzito ambao mara nyingi hukusudiwa kumuonya, kumuongoza na kumuadilisha binadamu. Kwa muonekano wa nje methali huwa na muundo wenye pande mbili. Upande mmoja unaeleza mazoea, tabia ya mtu au kitu juu ya utendaji wa jambo na upande wa pili unaeleza matokeo yatokanayo na mazoea hayo au tabia hiyo ambayo imeelezwa upande wa kwanza. Kwa mfano, *Ukimnunia jirani, uombe chumvi kwa nani*. Tunaona upande wa kwanza ni *Ukimnunia jirani* na upande wa pili ni *uombe chumvi kwa nani*. Data zilizokusanywa na mtafiti zimeonyesha kuwa katika nyumba za vijiji za Pemba methali zimejitokeza mara kadhaa katika kuta za nyumba hizo. Kwa mfano, *Mtaka cha mvunguni sharti ainame*ni moja kati ya methali zinazopatikana katika nyumba hizo ambao unalengo la kuhamasisha bidii ili mtu kufikia lengo alilolikusudia.

Mfano mwengine wa methali hizo ni *Ukiona vyaelea ujue vimeundwa*. Kupitia methali hii tunaoneshwa kuwa bidii imefanyika hadi kuona vitu vimefikia mafanikio. Baadhi ya watafitiwa waliohojiwa na mtafiti walisema kuwa maandishi hayo kwanza yameandikwa na mwenye nyumba kwa ajili ya kufanya bidii katika kazi ili hatimae kufanikiwa.

Vile vile, data zinaonyesha kuwa katika kuta za nyumba za vijijini kuna matumizi ya methali*Zimwi likujualo halikuli likakwisha.*Msomaji anaposoma methali hii ataelewa kuwa mwandishi alikusudia kuwataka wanajamii kuthamini ndugu wakaribu. Methali hii inakinzana na ile inayosema Kikulacho ki nguoni mwako ambayo inafichua kwamba kila siku adu wa mwanzo ni yule aliye karibu nawe.

Methali nyengine ni ile inayosema *Kila king`aacho si dhahabu*. Hii inamaanisha kwamba umbo la nje la kitu huwa halitoi picha halisi ya baadhi ya vitu hivyo. Msomaji wa methali hii anaweza akapata maana mbalimbali. Baadhi ya watafitiwa walisema inaweza ikawa si kila mwanamke mzuri na mrembo anafaa kuwa mwanamke bora katika ndoa. Wapo wanawake wazuri lakini huolewa kila siku na kuachwa kila siku kutokana na kukosa tabia nzuri. Usemi huu una dhima kubwa katika jamii ya kuonesha kwamba si kila kitu kizuri kilichopambwa kwa nje kinaweza kuwa na tabia nzuri.

Utafiti huu umebaini kuwa methali nyingi huandikwa katika nyumba za vijiji za Pemba. Zilizochambuliwa hapa ni baadhi tu ya methali hizo. Methali zina matumizi mengi. Pamoja na kuelezea ukweli fulani kuhusu maisha, hutumika kama fumbo, kejeli, kijembe, kuonyesha falsafa ya watu katika maisha yao, kuhimiza jambo,

kuonya, kutia moyo, kuelimisha na kupamba lugha (Kingei na wenzake, 2005: 35). Haya hufikishwa katika jamii kwa kutumia lugha ya ishara ambazo msomaji huweza kupata picha ya methali hizo kwa kutumia uhusiano ulipo kati ya ishara hizo na jamii. Kama nadharia ya Simiotiki inavyoonyesha kuwa Msimbo wa Kiishara unaweza kutumika ili kuonyesha maana zinazojidhihirisha kwa kutumia ishara ili kupata picha ya jamii husika.

### 4.2.7 Takriri

Takriri ni mtindo wa usemi ambao msemaji hurudia sauti, amofimu, neno au maneno yaleyale kwa lengo la kutia mkazo au kusisitiza jambo. Mawazo haya yanathibitishwa naKahigi na Mulokozi (1979) ambao wanaielezea takririkuwa ni uradidi, yaani urudiaji wa sauti, neno, kirai kishazi na hata sentesi katika kazi za kifasihi. Mbinu hii imekuwa ikitumiwa na wanafasihi kama kipengele muhimu katika kuifanya kazi zao kuwa na usanii huku zikiwa na athari fulani kwa jamii.

Data zilizokusanywa na mtafiti katika semi zinazoandikwa kwenye kuta za nyumba za vijiji Kisiwani Pemba zinaonyesha kuwa methali hizo zimekuwa zikitumia mbinu ya kisanaa ya takriri neno ambapo neno moja linarudiwa rudiwa ili kuweka mkazo katika maudhui yanayoibuliwa. Kwa hivyo, takriri huifanya hadhira iweze kutafakari kwa kina suala linalowasilishwa kwa kutumia takriri na hivyo kupata uzito wa maudhui. Kwa mfano, katika methali *Si mzizi wala shina matawi ndio fitina*kuna takiriri ya kitenzi kishirikishi *si* ambacho kinalenga kukanusha mawazo yanayoelezwa na kutilia mkazo *Matawi ndio fitina*.

Vile vile, katika semi hizo kuna matumizi ya takriri silabi ambazo huzifanya baadhi ya semi hizo ziwe na muundo wa ushairi. Kwa mfano, *Sema nao, cheka nao, kusema*

*ndio kazi yao*. Katika semi hii takriri silabi inajitokeza kwa kurudiwa rudiwa silabi inayojitokeza katika neno 'nao' na 'yao' ambapo silabi 'o' inarudiwa rudiwa. Aina hii ya takriri pia inajitokeza katika msemo `*Usijaze masusu kwa mambo yasiyo kuhusu*` ambapo silabi `*su*` inarudiwa rudiwa katika neno `*masusu*` na `*kuhusu*.`

Kwa kutumia Msimbo wa Kiishara unaopatikana katika nadharia ya Simiotiki ambao unahusishwa na jinsi ambavyo wasomaji wanavyovumbua maana ya kiishara katika kazi za kifasihi, mtafiti anavumbua namna waandikaji wa semi katika nyumba za vijiji za Pemba wanavyotumia mbinu ya takriri ili kujenga ishara zenye kutilia msisitizo wa yale wanayoyajadili.

## 4.3 Dhamira Zinazowasilishwa na Semi Zilizoandikwa katika za Nyumba za Vijijiza Pemba

Lengo mahusui la tatu la utafiti huu lilikuwa ni kutathmini dhamira zinazojitokeza katika semi zinazopatikana nyumba za vijiji za Pemba. Lengo hili liliongozwa na swali la utafiti lisemalo "ni dhamira zipi zinazopatikana katika semi zinazopatikana katika kuta za nyumba za vijiji za Pemba?" Fasihi inatumiwa kama kioo ambapo humulika vipengele vya maisha vya jamii inayohusika. Hivyo basi, data zilizokusanywa na mtafiti zimeonesha semi zilizoandikwa kwenye nyumba za vijiji za Pemba zina dhamira kadhaa kama zinavyojibainisha katika sehemu hii.

### 4.3.1 Kuburudisha

Semi zilizoandikwa katika nyumba za vijiji za Pemba zina dhamira ya kuburudisha wanajamii. Katika kufanikisha dhamira hii wanajamii huzitumia semi hizo kama kiliwazo kutokana na kero fulani ambayo wamekumbana nayo. Kwa hivyo, semi zilizoandikwa katika kuta za nyumba hutumika kama ni njia moja ya kujistraehesha

na kujifurahisha. Mfano wa semi hizo ni ule unaosema *Mchawi house* ambao una maana ya nyumba ya mchawi. Usemi huu unakuwa ni kiburudisho ambacho huibua kichekesho kutokana na kukengeusha uhalisia wa maisha ya Uswahilini ambako watu wenye tabia ya kufanya uchawi hawajibainishi hadharani lakini mwenye nyumba hii anaamua kutumia msemo huo.

Pia, usemi mwengine ambao unatumika kama ni njia ya kuburudisha ni ule unaosema "*Nyumba ya bilisi.*" Kupitia usemi huu tunaona namna jamii inavyoweza kuburudika kutokana namatumizi ya neno bilisi ambaye ni kiumbe chenye laana katika imani ya dini ya Uislamu na Ukiristo. Maamuzi ya kuandika msemo huu katika kuta za nyumba kunawafanya watu wafurahie kutokana na ukengeushi wa utamaduni wa jamii hiyo. Kutokana na utamaduni wa jamii msemo huo hautumiki katika maisha ya kawaida.

Pia, katika semi "*I love you*" kunapatikana dhamira ya kuburudisha. Hiini semi inayotumia maneno ya lugha ya Kiengereza ukiwa na maana ya "Nakupenda." Katika semi hiyo, msomaji anavutiwa na mseomo huo ambao unaibua hisia za upendo miongoni mwa wahusika. Kupitia Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji unampa nafasi mhakiki au msomaji wa kazi za fasihi kuibua maana kutokana na kile kinachoelezwa kuihukumu kazi hiyo kutokana na uzoefu alionao. Kwa kutumia nadharia hii msomaji anapata picha ya namna watumiaji wa misemo hii wanavyoitumia ili kufurahisha jamii.

### 4.3.2 Kuifunza Jamii

Dhamira nyengine inayojidhihirisha katika semi zilizoandikwa katika kuta za nyumba za vijiji za Pembani ile ya kuifunza jamii. Katika semi hizo tunabaini kuwa

kuna dhamira ya kuwafunza wanajamii ili wanajmii kuwa katika jamii yenye muelekeo uliobora na wenye kukubalika. Miongoni mwa semi zilizoandikwa katika kuta za nyumba katika jamii hiyoni ule unaosema *Pita na zako*. Kupitia msemo huo, jamii inaelimishwa umuhimu wa kutoshughulikia kila linalotokea katika jamii hasa lile ambalo halina mchango chanya katika jamii.

Pia, katika msemo unaosema *Maisha siri* una lengo la kuifundisha jamii kuhusu suala la maisha. Mafunzo yanayojitokeza hapa ni kwamba maisha ni suala la mtu binafsi, hivyo linabakia kuwa ni siri ya mtu anayehusika na maisha hayo. Kitendo cha kusimulia kila kipengele cha maisha kwa kila mwanajamii hakikubaliki. Hivyo kupata au kukosa kunatakiwa iwe ni siri ya mtu binafsi.

Aidha, msemo unaosema kuwa *Usimuogope mbwa mwenye meno, muogope jirani mwenye maneno*, unaifundisha jamii kuhusu uhusiano wa maisha miongoni mwa majirani. Msisitizo unaotolewa kupitia msemo huu ni kwamba majirani wawe na matumizi mazuri ya maneno ili kuimarisha uhusiano mwema. Kama inavyoelezwa kuwa maneno ndio msingi wa uhusiano huo. Kutokana na umuhimu huo, TAKILUKI (2002) katika shairi la *Ulimi* wanaeleza namna matumizi mazuri ya maneno yanavyoweza kumfanya mtu kuwa na mvuto kwa watu na kwa upende mwengine matumizi hayo ya maneno yanavyoweza kuharibu uhusiano na kuwafanya watu kuwa maadui.

Vile vile, kupitia msemo "*Ukimnunia jirani uombe chumvi kwa nani?"* kunajichomoza dhamira ya kuielimisha jamii kuhusu suala la ujirani mwema. Kila mwanajamii anasisitizwa kumtendea wema jirani yake. Hiyo ni desturi ambayo

inahimizwa na jamii na hata katika maandishi yanayohusiana na imani za kidini. Kwa mfano, kwa waumini wa dini ya kikristo, ndani ya Bibiliakitabu cha Warumi (uk. 13) inasema*pendo halimfanyi jirani jambo baya (Warumi aya ya 10) majirani hutendeana wema kama mtu anavyojitendea yeye mwenyewe*. Katika kazi za fasihi andishi, pia dhamira hii ya ujirani mwema imekuwa ikijadiliwa na baadhi ya waandishi wakiwa na lengo la kuhimiza ujirani mwema. Kwa mfano, Mbogo (2002) katika riwaya ya *Watoto wa Mamantilie* (2002) anamuonyesha namna mhusika Zenabu alivyomsaidia Zita, mtoto wa jirani yake baada ya kung`atwa na mbwa. Zenabu aliamua kumpeleka Zita hospitali ili kupata matibabu kutokana na wazazi wake hawapo nyumbani wakati lilipotokea tukio hilo. Katika kukosoa majirani ambao wanawafanyia ubaya majirani wao, kuna msemo ambao umenukuliwa katika kuta za nyumba za vijiji za Pemba ukieleza kwamba *Usimuogope mbwa mwenye meno, muogope jirani mwenye maneno.* Kupitia msemo huu majirani wanaonywa kuwa makini na kuchukua tahadhari kubwa kwa majirani wenye maneno machafu dhidi ya majirani wao.

Vile vile, data zilizokusanywa na mtafiti zinaonyesha kuwa misemo iliyoandikwa katika nyumba hizo zina dhamira ya kuwaelimisha wanajamii kuhusu falsafa ya mapenzi. Suala hili la mapenzi linajitokeza katika msemo unaosema *Wazuri haweshi* ambapo unalengo la kuwafundisha wanajamii kuwa watu wenye maumbo mazuri na ya kuvutia ni wengi katika jamii. Hivyo hawezi kutokea mtu kuweza kumaliza wazuri wote hasa katika mahusiano ya mapenzi nandoa. Kutokana na ukweli huo, data nyengine inayoshadidia dhamira hii ya mafunzo kuhusu mapenzi ni usemi unaosema *Tulia tuishi, wazuri haweshi.* Kupitia msemo huu wanandoa wanatakiwa

kutunza na kushughulikia maisha ya kuimarisha ndoa yao badala ya kutaka kukidhi ama kujitosheleza kimwili kutokana na mapenzi ya kila anayeonekana mzuri. Hili pia linakosolewa na Shaaban Robert (1951) katika riwaya ya *Kusadikika* anapohoji mwanamke mmoja anauzuri wa kiasi gani wa kuolewa na kila mtu?

Pia, zipo semi zilizoandikwa katika kuta za nyumba za vijiji za Pemba ambazo zinawaelimisha wanajamii kuhusu bidii katika kazi. Kwa mfano katika methali "Mtaka cha mvunguni sharti ainame" inatilia mkazo watu kufanya kazi ili kufikia malengo walionayo. Kwa kutumia methali hii jamii inatakiwa kujua kwamba mafanikio hayaji kama ndoto bali yanahitaji bidii. Kwa kutumia, msimbo wa Kiishara unaojitokeza katika nadharia ya Simiotiki kitendo cha kuinama ni kufanya bidii ya makusudi ili kufikia lengo lililokusudiwa. Aidha, "cha mvunguni" ni malengo na matarajio ambayo yanatarajiwa kufikiwa.

Semi nyengine ambayo inaweza kuingia katika tapo la semi zinazoifunza jamii ni methali isemayo "Mbaya halisi na wema hakosi." Kupitia methali hii, mafunzo yanayopatikana ni yale yanayolenga kuhamasisha uhusiano bora miongoni mwa wanajamii bila kutilia mkazo kasoro za kibinadamu zinazojitokeza miongoni mwao. Maisha ya binadamu na uhusiano wa wanajamii wengine ni kwamba kila mwenye kuonekana kuwa na ubaya, kwa upande mwengine ana matendo mazuri ambayo huweza kuwasaidia wanajamii.

Tunaporejelea nadharia ya Simiotiki kwenye msimbo wa Kiishara ambao unaangazia namna msomaji anavyovumbua maana za kiishara katika fasihi inayompa uhuru msomaji kupata picha ya kile kinachozungumzwa mtafiti amebaini kuwa semi hizo

zimekuwa na mafunzo yanayolenga kuijenga jamii. Aidha, kwa kutumia nadharia ya Mwitiko wa Msomaji mtafiti amebaini kuwa semi zilizoandikwa kwenye nyumba za vijiji za Pemba zinamfungamano mkubwa na maisha ya jamii kutokana na mafunzo yanayotolewa kuihusu jamii. Mawazo haya yanafungamna na yale ya Msokile (1992) anapoeleza kuwa nadharia ya Mwitiko wa Msomaji huikabili kazi ya fasihi kwa kuangalia jinsi inavyohusiana na mazingira ya kijamii.

### 4.3.3 Dhamira ya Kukosoa

Fasihi ni zao la jamii na kwa hivyo kile kinachojadiliwa katika kazi ya fasihi huihusu jamii. Kwa vile fasihi ni zao la jamii humwurika mazuri na mabaya ya jamii hiyo na kuyaeleza na hata kuyatolea mapendekezo. Mawazo haya yanaenda sambamba na mawazo ya Sengo (2009) ambayo yanasema kwamba fasihi hushughulikia matamu na machungu yaliyomo katika jamii husika. Kwa muktadha huo fasihi hutumika kama kipazasauti cha kuikosoa jamii. Data zilizokusanywa na mtafiti zinaonyesha kuwa semi zinazoandikwa katika nyumba za Pemba zinaikosoa jamii hiyo katika vipengele anuai. Kwa hivyo, semi hizo zinasawiri dhamira inayohusu kukosoa matendo ya wanajamii kama ifuatavyo:

Kwanza, kuna matumizi ya msemo unaoeleza hivi *Usimuogope mbwa mwenye meno muogope jirani mwenye maneno*. Kupitia msemo huu majirani wenye tabia ya kutotumia maneno vizuri wanakosolewa kutokana na tabia hiyo isiyokubalika. Hii ni tabia ambayo inaleta migogoro miongoni mwa wanajamii. Aidha, tabia ya majirani wanaotumia maneno vibaya wanaonekana kuwa hawana thamani na wanalinganishwa na mbwa lakini mbwa anakuwa na thamani zaidi kuliko jirani huyo. Kwa kutumia, nadharia ya Simiotiki kwenye Msimbo wa Ki-seme ambao

unampa fursa mhakiki kupata picha ya mhusika fulani wa kifasihi, ni kwamba picha inayopatikana kuhusu jirani mwenye maneno huwa jirani huyo anakuwa hana thamani katika jamii.

Aidha, zipo semi ambazo zina dhamira ya kutomnunia jirani. Miongoni mwa semi hizo niule unaosema *"Ukimnunia jirani uombe chumvi kwa nani?"* Kupitia msemo huu, majirani wanatakiwa wasiwe na chuki badala yake wajue kuwa majirani ndio wanaosaidiana pale mmoja wao anapokuwa na shida. Nadharia ya Simiotiki kwenye Msimbo wa Kiishara unatupatia picha ya kwamba chumvi inayoweza kuombwa kutoka kwa jirani ni namna majirani walivyo na tabia ya kusaidiana hivyo kitendo cha kuleta mgogoro miongoni mwao ni kuvunja uhusiano mwema.

Msemo mwengine unaolenga kuikosoa jamii ni ule unaosema *"Usijaze masusu kwa mambo yasokuhusu."* Kupitia msemo huo jamii inakosolewa kuhusu suala la kuchukua maneno kutoka upande mmoja na kuyapeleka katika upande mwengine kwa nia ya kuleta chokochoko ili kufanya watu wagombane. Msemo mwingine wenye dhamira iliyofanana na hii ni ule unaosema *"Kila uonalo wasema na hili kaseme."* Kitendo cha kujaza masusu na kitendo cha mtu kuona kila jambo akasema, ni kitendo cha kuchukuwa maneno ya uchochezi. Kwa kutumia nadharia ya Simiotiki kwenye Msimbo wa Kiishara kujaza masusu ni ishara ya maneno ya kufitinisha.

### 4.3.4 Mapenzi

Watu wengi leo hii wamejaa tamaa ya kutaka kufanya ngono na kila mtu. Watu hawa hujikuta wakidharau hata ndoa zao kutokana na kupenda ngono. Bwanga (2017) alipokuwa anakemea matendo ya ngono holela miongoni mwa wanajamii anaeleza

kuwa, kuna mambo unaweza kuyafanya kama kijana usione matokeo yake lakini yakakujengea mustakabali mbovu kwenye maisha yako ya baadae. Kwa mfano, mtu aliyezoea ngono holela katika ujana wake, anapoingia kwenye ndoa anajikuta hawezi kujizuia kufanya hivyo. Data zilizokusanywa na mtafiti zinaonyesha kuwa semi zilizoandikwa kwenye nyumba za vijiji za Pemba zimekuwa zikisawiri dhamira hii ya mapenzi. Kwa mfano, msemo unaosema "*Tulia tuishi, wazuri haweshi"* ama ule unaosema "*wazuri haweshi*" zinajadili dhamira ya mapenzi ambayo yanamuhusu mtu mwenye tamaa ya kutaka kufanya ngono na kila mtu. Kwa kutumia misemo hii, wale wenye tabia hiyo wanaelezwa kuwa mtu hawezi kufanya mapenzi na kila mzuri, kwani hao ni wengi na kamwe hawezi kuwamaliza. Ili kuonesha umuhimu wa mapenzi ya kweli wanajamii wamekuwa wakitumia msemo unaosema *"I love you"* ambao unatumia lugha ya Kiengereza ukiwa na maana ya "Nakupenda." Kwa kutumia msemo huu kunakuwa na ushadidiaji wa mapenzi miongoni mwa wahusika.

Vile vile, katika kujadili dhamira ya mapenzi zipo semi ambazo zinaonyesha kuwa mapenzi hukuzwa kwa mapenzi ya kila upande. Mfano wa semi hizo ni ule unaoeleza kuwa *Sina sifa ya jinni kumpenda asiyenithamini.* Kwa kutumia usemi huu jamii inajifunza kuwa suala la mapenzi si la upande mmoja tu. Kila mtu aliemo katika mapenzi inampasa amthamini mwenza wake. Mapenzi yanakuwa mithili ya pande mbili za sarafu moja. Ili kukamilika kwasarafu hiyo lazima kila upande uwepo na uwe umejitosheleza. Vivyo hivyo suala la mapenzi linahitaji kuthaminiana kwa kila uapnde kati ya pande mbili za wahusika.

Kwa ujumla mtafiti anaporejelea nadharia ya Mwitiko wa Msomaji amebaini kuwa nadharia hiyo inalandana na mawazo yanayojichomoza katika nadharia hiyo.Mtafiti

amehukumu misemo hii kutegemea mazingira ya jamii. Hivyo kutokana na msingi huo kinachojidhihirisha katika maisha ya jamii ni kwamba wapo baadhi ya wanandoa ambao hujikuta wakitaka kufanya mapenzi na kila mtu jambo ambalo huchochea migogoro katika ndoa zao na kuendeleza ngono holela. Ukweli ni kwamba watu wenye tabia hiyo huangukia katika wimbi la wenye kuhatarisha maisha yao na familia zao kutokana na kueneza ugonjwa wa Ukimwi kutokana na kufanya ngono holela. Aidha, baadhi yao hujikuta wakiingia katika migogoro ya ndoa. Kama inavyoelezwa Buliba na wenzake (2017) kwamba moja ya kichocheo cha migogoro katika ndoa ni baadhi ya watu kuwa na mapenzi ya nje ya ndoa. Aidha, TAKILUKI (2002) katika diwani ya *MalengaWapya* (2002) shairi la "Kwa Nini?" anakosolewa muume aliye katika ndoa ambaye anaamua kuacha kuihudumia ndoa yake nakuamua kushughulikia wanawake wengine ili kufanya nao mapenzi.

### 4.3.5 Kukejeli

Kejeli ni kueleza kitu kwa njia ya kudhihaki. Watu wanapokejeli kitu hulenga kukidogesha au kukidharau. Uchambuzi wa data za utafiti huu umeonesha kwamba zipo baadhi ya semi zilizoandikwa katika kuta za nyumba katika jamii ya Wapemba kisiwani Pemba zenye kuisawiri dhamira ya kukejeli. Kwa mfano, dhamira ya kukejeli imejitokeza katika semi inayoeleza *Bure munajipa dhiki kujikwaa navizingiti linalowakera ni lipi?*Kwa kutumia usemi huu, wanakosolewa wanajamii wenye tabia ya kuchunguza ya watu wengine. Msemo huu hutumika kutoa picha ya mtu ambaye hutumia muda wake mwingi kwa lengo la kuchunguza ama kusikiliza mazungumzo ya watu wengine akiwa na lengo baya.

Vile vile, katika msemo unaosema *Mwajenga nyumba zenu hamuzitii penu mutasema wapi vichakaa vyenu?* Katika dondoo hii kejeli inajidhihirisha kutokna na namna msemo huo unavyolenga kuwakejeli wale wenye tabia ya kusengenya. Kutokana na tabia hiyo wanaambiwa kuwa wajenge nyumba zenye penu (baraza upande wa pembenni mwa nyumba) ili kukaa na kuanza kuwasengenya wengine. Kejeli mara nyengine huweza kujitokeza kama swali ambapo watu wanauliza ili kumkejeli yule anayefanya jambo hilo kama inavyojidhihirisha katika mfano huo.

Aidha, dhamira ya kukejeli inajidhihirisha katika msimu usemao *Utajiju.* Huu ni msimu ambao katika jamii ya Wapemba una maana ya kumkejeli mtu ambaye amefanya jambo ambalo halikubaliki kufanyika katika jamii hiyo. Kwa kutumia msimu huo wanajamii wanakejeliwa kutokana na kutenda matendo ambayo yanawaingiza katika matatizo ama majanga. Hivyo mtu anapofanya jambo hilo na kujikuta katika matatizo anaambiwa kuwa atajijua mwenyewe kutokana kutokuwa makini.

Msemo mwengine ambao una sawiri dhamira ya kukejeli ambao unapatikana katika baadhi ya nyumba za vijiji za Pemba ni ule unaosema "*Kila uonalo wasema na hili kaseme.*" Katika dondoo hii tunaoneshwa namna wanajamii wenye tabia ya kusema kwa ubaya kila jambo wanaloliona wanavyokejeliwa na kuelezwa kwa njia ya kukejeli kuwa waendelee kufanya hivyo wasisite.

Kupitia nadharia ya Mwitiko wa Msomaji mtafiti anapata ujasiri wa kuungana na wale wanaoandika misemo hiyo katika kuta za nyumba yao ili kukejeli baadhi ya matendo ya wanajamii ambayo hayalengi kujenga jamii endelevu. Dhamira ya

kukejeli inajidhihirisha kama msingi mkuu wa athari zinazopatikana katika semi zinazoandikwa kwenye kuta za nyumba za Kisiwani Pemba. Matumizi haya yanaakisi maisha halisi ya jamii hiyo ambayo yanahitaji kukejeliwa ili kutoyaendeleza na kuendelea kuleta athari hasi. Kwa mtazamo huo ndio maana Njogu na Mwai (1993) wanaeleza kwamba fasihi ni zao la jamii na kile kinachojadiliwa kimo katika jamii. Kwa mantiki hii kejeli zinazopatikana katika semi hizo ni akisiko la wanajamii ambao wamechoshwa na matendo yasiyofaa.

### 4.3.6 Itikadi

Dhamira ya itikadi huhusu muelekeo wa kijamii pamoja na msimamo wa mtunzi katika kazi za fasihi. Mulokozi (1996) anaeleza kwamba dhima ya kiitikadi inategemea muktadha wa jamii inayohusika pamoja na nafasi ya mtunzi katika jamii hiyo na msimamo wake kuhusiana na migogoro na wakati wake. Hivyo fasihi inaweza kutumiwa ili kuendeleza itikadi ya tabaka linalotawala. Anaendelea kueleza kwamba jamii yenye mgawanyiko wa kitabaka au kijumuia hugawanyika pia kiitikadi. Itikadi ya kiutawala hugongana pia naitikadi ya wale wanaotawaliwa. Pamoja na mawazo hayo ya Mulokozi data zilizokusanywa na mtafiti zimebainisha kuwa itikadi ya imani ya Mungu imekuwa ikijidhihirisha katika semi zinazoandikwa katika kuta za nyumba za vijiji za Pemba. Kwa mfano, moja ya semi yenye itikadi hiyo ni ule usemao *Mungu Mkubwa.* Kupitia usemi huo jamii inaamini kwamba Mwenyezi Mungu ndie mwenye uwezo wa kila kitu hivyo hata matatizo yanapojitokeza yeye ndiye anayetoa msaada wa kuyatatua.

Vile vile, kuna msemo ambao unasema *Piga hodi mara tatu*. Huu ni msemo ambao umekuwa ukiandikwa juu ya mlango ama pembeni ya mlango wa kuingilia katika

baadhi ya nyumba za jamii ya Wapemba. Msemo huu unawataka wanajamii wawe na tabia ya kubisha hodi mara tatu kabla ya kuingia katika nyumba ambayo simo anamoishi. Hii ni itikadi inayoambatana na imani ya mafunzo ya dini ya Uislamu ambayo katika kitabu kitakatifu cha Qurani kinaamrisha watu kutoingia katika nyumba ambayo si yao hadi pale watapobisha hodi na kabla ya kuingia wawatolee salamu watu wanaoishi katika nyumba hiyo. Aidha, iwapo mtu ataambiwa arudi yaani asiingie inampasa arudi kutokana na ushahidi wa hadithi inayosema "Alstiidhanu thalatha…"

Kwa vile suala la itikadi pia huhusu kipengele cha utabaka, semi zinazoandikwa katika kuta za nyumba za vijiji za Pemba zimekuwa zikisawiri itikadi hiyo ya kitabaka. Mathalani, msemo unaosema `*Warambe wao tu*` unalenga kuonyesha namna baadhi ya wanajamii wanavyofaidika na matunda ya uhuru, huku tabaka la chini linavyoendelea kuteseka kutokana na hali ngumu ya maisha. Hivyo msemo huo umetumika kukosoa mgawanyo huo wa kitabaka unaoikabili jamii ambayo ililenga kudai uhuru ili kuleta usawa wa kimaendeleo miongoni mwa wanajamii. Maisha haya ya utabaka ni moja kati kichocheo kinachorudisha nyuma ustawi wa wanajamii. Hili linathibitishwa na TAKILUKI (2002) katika diwani ya *Malenga Wapya* kwenye shairi la "Hali Halisi" katika shairi hilowatunzi wanaonyesha kwamba kupatikana kwa uhuru wa bendera katika nchi za bara la Afrika hakujaleta nafuu ya maisha kutokana na watu wanavyoendelea kuishi katika hali ngumu ya maisha ambapo chanzo kikuu ni kutokana na tatizo la utabaka. Katika shairi hilowatunzi wanatumia ishara ya `mshumaa unaowaka lakini kiza kinazidi` ili kutoa picha ya uhuru uliopatikana lakini matatizo yakiendelea katika bara hili kutokana na kuwepo kwa utabaka.

Tunaporejelea nadharia ya Mwitiko wa Msomaji inayompa uhuru msomaji kuweza kuisoma, kuielewa na kuihakiki kazi ya fasihi kadri ya uelewa na tajiriba ya usomaji wake kuhusu masuali mbalimbali ya kijamii mtafiti wa kazi hii analieleza suala la itikadi kama linavyojidhihirisha katika semi zilizoandikwa katika kuta za nyumba za jamii hiyo linalandana na hali ilivyo katika jamii ya Wapemba. Kwa uzoefu wa mtafiti na tajiriba alizonazo mtafiti anaihakiki jamii kwa kusema kwamba jamii ya Wapemba kama zilivyo jamii nyingi inazo itikadi zilizofungamana na imani ya uwezo mkuu wa Mungu ambapo huona kuwa ndio kimbilio lao katika kupata utatuzi na msaada kwa mambo kadhaa yanayoikabili jamii. Aidha, sula la matabaka bado ni changamoto inayoikabili jamii hiyo. Upo mpaka kati yatabaka la wenye nacho na wale wasonacho. Maingiliano kati ya matabaka haya yana mipaka yake. Mpaka huo umejengwa na ile hali ya tabaka moja kuwa na uwezo wa kifedha na tabaka jengine kutokuwa na uwezo huo. Mulokozi (1996) anasema kuwa jamii yoyote huwa na matabaka. Hivyo fasihi imekuwa ikitumiwa ili kuendeleza ama kukosoa tabia ya tabaka fulani. Kwa mantiki hiyo, pamoja na kuwa maisha ya jamii nyingi yamejikita kitabaka, lakini katika semi zinazoandikwa katika kuta za nyumba za vijiji za Pemba hazilengi kuendeleza utabaka huo bali kuonyesha hali ilivyo ili kuondokana nayo.

### 4.3.7 Uchumi

Moja ya dhamira ya semi zinazoandikwa katika nyumba za vijiji za Pemba ni kuonyesha suala la uchumi. Baadhi ya semi hizo hutumika zikiwa na dhamira za kibiashara. Kwa mfano, msemo unaosema *Al-Jazira halua* ambao unamaana ya halua yenye ladha ya Al-Jadhira unalengo la kuwavutia watu kununua halua hiyo

kwa lengo la kuzidisha biashara. Pia, katika uwanja huu wa biashara zipo semi kama vile *Haji Kiua na Haji Chandarua Barning CD.* Msemo huu umeandikwa kwenye ukuta ambao kuna kituo cha kukodisha na kuuza CD ambazo hutumiwa na wanajamii.

Vile vile, semi zilizochorwa katika nyumba za vijiji za Pemba zinatumiwa na makampuni makubwa ya biashara kama vile makampuni ya simu za mkononi ili kuwavutia watumiaji wake. Kwa mfano, data zinaonyesha katika baadhi ya kuta za nyumba za jamii hiyo kunaonekana misemo kama vile "Sapuka na Zantel." Msemo huu unalenga kushajiisha watumiaji wa simu za mkononi kujiunga na mtandao huo na kutumia huduma zake. Pia, kuna msemo unaosema *Easy na Eze Pesa*. Msemo huu umekuwa ukiandikwa katika kuta za nymba ambazo zinatoa huduma za kutuma na kupokea pesa kupitia mtandao wa Zantel. Lengo kuu la msemo huu ni kutaka kueleza jamii kwamba utumaji na upokeaji wa pesa kupitia mtandao wa Zantel ni rahisi.

Pia, msemo unaoeleza *Laki si pesa* unaonyesha namna thamani ya pesa ya Tanzania ilivyoshuka thamani ikilinganishwana pesa za kigeni kama vile dola. Kutokana na kushuka kwa thamani ya sarafu ya Tanzania hali ya uchumi imekuwa ni ngumu. Hapo kabla laki moja iliweza kuwa na thamni kubwa ukilinganisha na sasa. Hali hii imewaathiri wafanyabiashara hasa wafanyabiashara ndogo ndogo na jamii kwa ujumla ikiwa ni pamoja na bidhaa kupanda bei mara kwa mara.

Kwahivyo mtafiti wa kazi hii kupitia nadharia ya Mwitiko wa Msomaji inayompa uhuru msomaji kama inavyoelezwa na Njogu na Chimerah (1999) kuweza

mtumiaji wa nadharia ya Mwitiko wa Msomaji hutoa fursa kwa msoamji kuisoma, kuielewa na kuihakiki kazi ya fasihi kadri ya uelewa na tajiriba ya usomaji wake kuhusu masuali mbalimbali ya kijamii, mtafiti wa kazi hii anaishauri jamii kwa kuiambia kwamba semi zinazoandikwa katika kuta za nyumba katika jamii hiyo zina dhamira muhimu katika kufikia lengo la uchumi hasa linalohusu masuala ya kibiashara katika kutangaza na kuhamasisha upatikanaji wa bidhaa na huduma na hatimae kupata faida.

### 4.3.8 Wivu

Wivu ni hisia za mtu ambazo humfanya awe makini zaidi katika kulinda penzi lake dhidi ya mpenzi wake. BAKIZA (2010) wanaeleza kuwa wivu ni hisia ya mtu kukasirika kutokana na kuhisi au kubaini uhusiano wa kimapenzi uliopo baina ya mpenzi wake na mtu mwengine. Wanaendelea kueleza kuwa mara nyengine wivu huweza kuwa ni tabia ya mtu kumlinda na kumfuatilia mpenzi wake kwa hofu ya kunyang`anywa na mtu mwengine. Data za utafiti huu zimebaini kwamba baadhi ya semi zilizoandikwa katika nyumba za vijiji za Pemba zinasawiri dhamira ya wivu hasa ule unaojikita kati ya mapenzi ya mtu na mtu.

Moja kati ya semi yenye kuibua dhamira ya wivu ni ule unaosema *Mimi ni wako mwengine hatotokea.*Katika msemo huu tunapata dhamira ya wivu miongoni mwa wapendanao. Kwa kawaida msemo huo hutumiwa na wanawake katika jamii ya Pemba na Uswahilini kwa ujumla ili kuthibitisha kuwa hakuna mtu mwengine ambaye anaweza kuingilia penzi miongoni mwao. Hivyo kwa kutumia msemo huo mwanamme anatakiwa atulize moyo wake na asiwe na wivu wa kuchupa mipaka wa kutomuamini mwenza wake.

Suala la wivu pia linajidhihirisha kupitia usemi unaosema *Usimuonee wivu jirani.*Kupitia usemi huu jamii inapewa wosia wa namna ya kuishi na majirani bila kushutumiana kwa kuoneana wivu katika masuala ya mapenzi. Hii ni kwa sababu jirani ni mtu muhimu sana katika jamii. Kutokana na umuhimu wake katika mahusiano ya kijamii Waswahili husema kuwa *Jirani ndie ndugu.*Hili linajidhihirisha kutokana na kwamba majirani hushirikiana katika masuala ya kijamii yanayohusu raha na shida kama vile harusi na misiba.

Suala la wivu miongoni mwa wanajamii ni sula muhimu sana ambalo kwa ujumla mtafiti anaweza kusema kuwa limelandana na nadharia ya Mwitiko wa Msoamaji. Suala hili ni miongoni mwa masuala yanayoendana na utamaduni katika jamii ya Wapemba. Kwa uzoefu wa mtafiti ni kwamba wivu usiokuwa na mipaka huwa unasababisha madhara makubwa kwa wanandoa na jamii kwa ujumla. Baadhi ya ndoa huvunjika kutokana na kutawaliwa na wivu usio na mipaka jambo ambalo hupelekea kushutumiana na kutoaminiana. Aidha, wakati mwengine wivu husababisha mifarakano na hata mapambano. Wapo wanaopigana na kuathiriana na mara nyengine hata kusababisha vifo kutokana na sababu ya wivu. Hivyo pamoja na kwamba wivu ni tabia ya kila mtu kama anavyoeleza p`Biteki (1984)katika kitabu cha *Song of Lawino and Song of Ocol* katika shairi la “The Woman With Whom I Shere My Husband” ambapo mhusika Lawino anakosoa tabia ya Okoli kumpenda Tina, mwanamke anayeiga mitindo ya Kimagharibi kama vile uvaaji wa mawigi, matumizi ya rangi za midomo, uvaaji wa nguo fupi na kadhalika ambazo hazimfanyi avutie, inapasa jamii iwe makini kuhusu suala la wivu.

### 4.3.9 Usimamizi wa Haki

Tunaposema kuwa haki ya binadamu tuna maana kuwa mtu anahitaji kupatiwa haki hiyo kwa sababu ni binadamu. Miongoni mwa haki hizo ni kuishi, kupata mahitaji muhimu kama vile kula, kunywa, kivazi, kuchanganyika na watu katika jamii, kupata elimu, haki ya kulindwa na sharia ili asidhuriwe na nyengine nyingi. Data zilizokusanywa na mtafiti zimeonyesha kuwa semi zilizotafitiwa zinaibua dhamira ya haki. Kwa mfano, msemo unaosema kuwa *`Haki ya mtu haipotei*.` Katika msemo huo dhamira ya haki inaibuluwa na kutiliwa msisitizo kwamba vyovyote iwavyo mtu ataipata haki yake. Ili kushadidia mtazamo huo, jamii ya Wapemba imekuwa ikitumia msemo usemao `*Haki haizami huelea*` kwa maana ya kwamba haki ya mtu hubakia kuwa ni haki yake na iko siku huipata. Mara nyengine imani hii huambatana na imani ya kidini ambapo waumini wengi wa dini ya Uislamu huamini kuwa haki ya mtu huwa haipotei kwani iko siku Mwenyezi Mungu atairudisha kwa yule anayepasa kupewa haki hiyo.

Aidha, utafiti umebaini kuwepo kwa msemo unaosema*Malipo ni duniani, Akhera kwenda hesabu* ambao ni msemo mwengine unaopatikana katika nyumba za vijiji za Pemba unaosawiri dhamira ya haki katika jamii. Katikamsemo huo, kunasawiriwa uhalisia wa maisha katika suala la haki. Msemo huo kama zilivyo semi zilizobainishwa hapo juu katika kipengele hiki cha haki, unaonyesha mchomozo wa kiimani kuhusu suala la haki miongoni mwa wanajamii na katika maisha ya kila siku. Imani hii ni ile inayoonyesha kuwa watu huanza kulipwa hapa hapa katika maisha ya dunia kabla ya mtu huyo kufikwa na umauti. Maisha ya baada ya kifo yatahitimisha kwa kuonyesha kila kitu ambacho mtu amekifanya katika maisha ya dunia.

Kwa uzoefu wa mtafiti, huku akiongozwa na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji inayompa uhuru msomaji kuweza kuisoma, kuielewa na kuihakiki kazi ya fasihi kadri ya uelewana tajiriba yausomaji wake kuhusu masualambalimbali ya kijamii, ameona kwamba suala la haki kama linavyojadiliwa katika semi zilizoandikwa kwenye nyumba za vijiji za Pemba linalandana na nadharia ya Mwitikko wa Msomaji. Kwa muktadha huo mtafiti amepata fursa ya kutoa maoni yake kwa kusema kwamba, katika jamii ya Wapemba kama zilivyo jamii nyingi ulimwenguni bado suala la haki limekuwa ni changamoto. Hata hivyo, kila mmoja anapaswa atambue kwamba haki ndio suala la msingi katika maisha ya kila mwanajamii. Pia, haki inasifa ya kutopotea na hubakisha athari katika maisha ya mtu hapa duniani na maisha ya baadae ya Akhera. Kwa sababu hiyo, Massoud (2017) anasema kuwa jamii inapaswa kutekeleza haki bila ya kujali suala la kiutabaka. Ili kutekeleza haki Massoud anakosoa maamuzi yoyote yanayohusu jamii ambayo yanashirikisha tabaka tawala tu bila kushiririkisha matabaka mengine ya kijamii.

## 4.4 Hitimisho

Sura hii inahusu uwasilishaji na uchambuzi wa data za utafiti. Katika sura hii kuna sehemu tatu ambapo sehemu ya kwanza imefanya uwasilishaji wadata zinazohusu kuzibainisha semi zinazoandikwa semi zilizoandikwa katika nyumba za vijiji za Pemba. Sehemu ya pili inachambua data zinazohusu lugha katika semi hizo nasehemu ya tatu inafanya uchambuzi wa data zinazohusu dhamira zinazopatikana katika semi zilizotafitiwa. Kwa ujumla baada ya kufanya uwasilishaji na uchambuzi wa data,mtafiti aliweza kujibu maswali ya utafiti huu. Hivyo basi, sura inayofuata inahusu muhutasari, hitimisho na matokeo ya utafiti huu.

# SURA YA TANO

# MUHUTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Hii ni sura ya tano na ya mwisho katika utafiti huu. Sura hii ina sehemu ndogo ndogo tatu. Sehemu ya kwanza imewasilisha muhtasari wa tasnifu hii, sehemu ya pili ni hitimisho la utafiti ambapo katika sehemu hiyo matokeo ya utafiti huu yamebainishwa na mwisho kuna sehemu inayotoa mapendekezo ya utafiti huu.

## 5.2 Muhutasari wa Tasinifu

Utafiti huu ulikuwa na lengo la kuchunguza semi zinazoandikwa katika nyumba za vijijiza Pemba. Semi zilizotumika ni zile tu ambazo zilikusanywa na mtafiti ambazo zimeandikwa kwenye nyumba za vijiji za Pemba. Hii ni kusema kuwa semi nyengine ambazo zinapatikana katika mazingira kama vile maandishi ya kanga, fulana, kuta za vyoo, vyombo vya usafiri wa baharini na nchi kavu, vipeperushi nakadhalika hazikutumika kama sehemu ya data za utafiti huu.

Utafiti huu ulikuwa na malengo mahususi matatu ambapo lengo mahususi la kwanza lilikuwa ni; “Kuzianisha semi zilizochorwa katika nyumba za vijiji za Pemba.” Lengo hili liliongozwa na swali la utafiti lisemalo; “Ni semi zipi zilizoainishwa katika kuta za nyumba za vijiji za Pemba?` Lengo mahususi la pili lilikuwa ni “Kubainisha matumizi ya lugha katika kuta za vijiji za za Pemba.` Lengo hili liliongozwa na swali la utafiti lisemalo “Ni matumizi yepi ya lugha yaliyobainishwa katika semi zinazopatikana katika kuta za nyumba za vijiji za Pemba?` Na lengo mahususi la tatu lilikuwa ni “Kutathmini dhamira zinazojitokeza katika semi zinazopatikana katika kuta za vijiji za Pemba.” Lengo hili liliongozwa na swali la

utafiti lisemalo “Ni dhamira zipi zilizojitokeza na kutathminiwa katika semi zinazopatikana katika kuta za nyumba za vijiji za Pemba?”

Tasnifu hii ina jumla ya sura tano. Sura ya Kwanza ni sura ya utangulizi ambayo inaeleza mambo ya msingi yanayohusu utafiti huu. Katika sura hii mtafiti amebainisha na kueleza usuli wa mada ya utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti na muundo wa tasnifu.

Sura ya pili inahusu mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa nadharia. Sura hii inasehemu ya utangulizi, dhana muhimu katika utafiti huu ambazo ni utangulizi wa sura, dhana ya dhamira, vipengele vya lugha ya kisanaa, mapitio ya maandiko kuhusu matumizi ya lughana pengo la utafiti. Mwisho sura hii imeeleza nadharia Mwitiko wa Msomaji na Simiotiki ambazo zimeongoza utafiti huu.

Sura ya tatu ya utafiti imeelezea mbinu za kukusanyia data zilizotumika katika utafiti huu. Vipengele vilivyoelezewa katika sura hii ni usanifu wa utafiti, eneo la utafiti na walengwa wa utafiti. Vipengele vyengine ni sampuli na mbinu za usampulishaji. Pia, sura hii inaelezea mchakato wa ukusanyaji wa data na uthabiti, kuaminika na maadili ya utafiti.

Sura ya nne imefanya uchambuzi na uwasilishaji wa data za utafiti huu. Sura hii imegawanyika katika sehemu ndogo ndogo tatu. Sehemu hizo zimepangwa kutegemea malengo ya utafiti huu. Sehemu ya kwanza iliwasilisha data za utafiti zinazohusu kubainisha semi zinazoandikwa katika kuta za nyumba za vijijini katika jamii ya Wapemba. Sehemu ya pili ni uwasilishaji wa data zinazohusu dhamira

zinazopatikana katika semi zinazoandikwa katika kuta za nyumba za ya jamii ya Wapemba. Mwisho, sura imefanya uchambuzi na uwasilishaji wa vipengele vya lugha katika semi zichorwazo kwenye kuta za nyumba za vijijini na namna vipengele hivyo vinavyoibua dhamira katika jamii ya Wapemba.

Sura ya tano imehitimisha kwa kutoa muhutasari wa utafiti, matokeo ya utafiti na mapendekezo. Sura hii inaeleza kwa muhtasari kile kilichogunduliwa na matafiti. Maswali yote matatu yaliyoongoza utafiti huu yanaelezwa majibu yake kwa ufupi kama ilivyobainishwa na kugunduliwa katika sura ya nne ya tasnifu hii. Hivyo basi, matokeo ya utafiti huu yalikuwa kama ifuatavyo:

## 5.3 Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu ulikuwa na malengo matatu ya utafiti. Kukamilika kwa utafiti huu kumaetupa matokeo kama yafuatayo:

### 5.3.1 Lengo Mahususi la Kwanza

Lengo mahsusi la kwanza la Utafiti huu lilikuwa ni: "Kuzianisha semi zinazopatikana katika nyumba za vijiji za Pemba." Lengo hili liliongozwa na swali la utafiti lisemalo; "Ni semi zipi zilizoainishwa katika nyumba za vijiji za Pemba?

Matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwa semi zilizoandikwa kwenye nyumba za vijiji za Pemba zinaweza kuwekwa katika makundi ya semi zenye kuonyesha utabaka, kuhimiza mshikamano, kuonyesha imani, kuhamasisha kazi, kukosoa, kukejeli, kuonyesha utamaduni, mapenzi na kuifunza jamii.

### 5.3.2 Lengo Mahususi la Pili

Lengo mahususi la pili la utafiti huu lilikuwa ni: “Kubainisha matumizi ya lugha katika semi zinazopatikana katika nyumba za vijiji za Pemba.` Lengo hili liliongozwa na swali la utafiti lisemalo “Ni matumizi yepi ya lugha yaliyomokatika semi zinazopatikana katika nyumba za vijiji za Pemba?` Matokeo ya utafiti huu yalionesha kuwa semi zinazopatikana katika nyumba za vijiji za Pemba zinatumia lugha ya lahaja, balagha, kejeli, tashihisi, misemo, methali na takiriri.

### 5.3.2 Lengo Mahsusi la Tatu

Lengo mahsusi la tatu la utafiti huu lilikuwa ni: “Kutathmini dhamira zinazojitokeza katika semi zinazopatikana katika nyumba za vijiji za Pemba.” Lengo hili liliongozwa na swali la utafiti lisemalo “Ni dhamira zipi zinazojitokeza katika semi zinazopatikana katika nyumba za vijiji za Pemba?” Matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwa semi zinazoandikwa kwenye nyumba za vijiji za Pemba zinaibua dhamira za kuburudisha, kuifunza jamii, kukosoa, mapenzi, kukejeli, itikadi, uchumi, wivu na usimamizi wa haki.

## 5.4 Hitimisho

Utafiti huu ulilenga kuchunguza semi zilizoandikwa kwenye nyumba za vijijiza Pemba. Matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwa semi hizo zinaibua dhamira kadhaa ambazo zinaihusu jamii. Wanajamii huzitumia semi hizo ili kuonyesha yale yaliomo katika nyoyo zao kama yanavyojitokeza katika maisha yao ya kila siku. Aidha, katika semi hizo kunajidhihirisha tamu na machungu waliyonayo wanajamii kutokana na muelekeo wa maisha ya kila siku. Mwisho, utafiti huu umebaini kuwa ingawa semi hizo zinajikita katika utanzu wa semi kama kipengele cha fasihi

simulizi, lakini ndani yake kuna vipengele vya lugha kama vile matumizi ya lahaja, balagha, kejeli, tashihisi na takiriri ambavyo hutumika kuibua dhamira zilizokusudiwa na wanajamii wanaozitumia semi hizo.

## 5.5 Mapendekezo ya Utafiti

Kwa watafiti wasomi wanaotegemewa na taifa, ni jukumu lao kufanya tafiti zaidi juu ya semi nyengine zinazopatika katika jamii ya Wapemba. Tafiti hizo zinaweza kujikita kwenye semi zinazoandikwa katika vazi la fulana, semi za kwenye gari za usafiri wa barabarani, semi zinazoandikwa kwenye vijiwe vya mazungumzo nakadhalika.

Vile vile, jamii inapaswa kuzitilia mkazo na kufanya uchambuzi wa kina kuhusu dhamira zinazopatikana katika semi zinazoandikwa katika kuta za nyumba za vijijini katika jamii ya Wapemba. Mkazo huo unaweza kutilia maanani jinsi dhamira zinazoibuliwa kupitia semi hizo ili kuirekebisha ama kuiendeleza jamii ili kujenga jamii mpya endelevu.

## MAREJELEO

Ali, K. H. (2018). *Dhima ya Majina katika Vyombo vya Uvuvi kwa Jamii ya Watumbatu*. Tasnifu ya Uzamili katika Kiswahili katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Enon, J.C. (1998). Educational Research; Statistics and Measurement. Kampala: Makerere University Press.

Faki, M. H. (2018). *Matumizi ya Lugha Tandawazi katiaka Mitandao ya Kijamii: Changamoto katika Lugha ya Kiswahili.* Tasnifu ya Uzamili MA-Kiswahili katika Chuo Kkikuu Huria cha Tanzania.

Gaichu, M. N. (2016*). KuchunuzaSitiari Dhanfu Katika Methali za Kiswahili-Mtazamo wa Nadharia ya Uhusiano.* Tsnifu ya Uzamili ya MA-Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Nairibi.

Hassan, H. A. (2017). *Kuchunguza Fasihi ya Majina ya Mitaa Mjini Unguja.* Tasnifu ya Uzamili MA-Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Jilala, H. (2016). *Misingi ya Fasihi Linganishi.* Dar es Salam: Daud Publishing Company

Julia, W. (2013). *Kanga kama Salijili Maalumu ya Kisanii na Mawsiliano*. Tasnifu ya Uzamili MA-Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Moi.

Juma, A. R. (2015). *Methali za Kswahili ilizoachwa: Sababu na Athai zake kwa Jamii*. Tasnifuya Uzamili MA-Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dodoma

Juma, N. (2016). *Semi Zilizoandikwa Kwenye Vyombo vya Safari vya Baharini Kisiwani Pemba.* Tasnifu ya Uzamili MA-Kiswahili katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Kahmis, S. A. M. (1983). Nafasi ya Fsihi Simulizi katika Jamii ya Tanzania. Katika Jarida la Mulika Na. 15 uk. 3-13.

Khatib, T. O. (2017). *Dhamira Zijengwazo na Taswira katika Methali za Wapemba*. Tasnifu yaUzamili MA-Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar.

Kipacha, A. (2014). *Misemo katika Lugha za Magari: Divai Mpya? Katika Jarida la Swahili* Forum Na. 21, uk. 104-121.

Kombo, D. K & Tromp, D. L. (2006). *Proposal and thesis Writing*. *An Introduction.* Nairobi: Paulines Publications Africa.

Kothari, C. R. (2008). *ResearchMethodology; Methods and Techniques*. New Delhi: New Age. International Publishing Limited.

Maitaria, J. N. (2012). *Uainishajiwa Ushairi wa Kiswahili kwa Kutumia Kigezo cha Methali.* Katika Mulika Na. 31, uk. 89-104.

Mahenge, P. (2009). *Semi zitumikazo kwenye tiketi za daladala*, *Mulika* Na 29 na 30. TATAKI.

Massamba, M. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Migpdela, W. (2017). *Dhamra za Maandishi ya Kuta za Vyooni* Jijini Dar es Salam.Katika Jarida la Mkwawa Journala of Education Na. 1 uk. 1-8.

Mtesigwa, G. K. (2013). *Kuchunguza Matumizi ya Methali katika Jamii ya Wanyiramba*. Tasnifu ya Uzamili MA-Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Tanzania.

Mulokozi, M. M. (1989). *Tanzu za Fasihi Simulizi. Mulika* 21:1-24, Dar es Salaam: TUKI.

(1996). *Fasihi ya Kiswahili* Chuo Kikuu Huria Cha Dar –es-Salamu.

Msuya, P. A. (1977). *Fasili ya Methali.* Katika Jarida la Mulika, Na. 9 uk. 29-31

Ndungo, C. W. na Mwai, W. (1991). *Kiswahili Studies*: Part Two. Nairobi: University of Nairobi

Ndungo, C. M. & Waful, R. M. (1993). *Tanzu za Fasihi Simulizi*. Nairobi: University of Nairobi Press.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Panneerselvam, R. (2012). *Research Methodology*. New Delh: PHI Learning Pivate Limited

Sengo T.S.Y.M. (2009). *Sengo na Fasihi za Kinchi.* Dar es Salaam: AERA Kiswahiki Research Products

Simyu, W. F (2011). *Kitovu cha Fasihi Simulizi.* Mwanza: Serengeti Education Publishers Ltd.

Skuni, M. M. (2018). *Kuchunguza Jinsi Nahau za Kiswahli Sanifu ZinavyokwamishaMawasiliano Fanisi kwa Wageni wa Lugha.* Tasnifu ya Uzamili MA-Kiswahili katika chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Taasisi ya Ukuzaji Mitaala (1988). *Kiswahili Sekondari*. Dar es Salaam: TUMI.

Timothy, K. M. (2016). *Maana ya Usemi na Mazungumzo katika Mitandao ya Kijamii HususanFacebook na Twetter.* Tasnifu ya Uzamili MA-Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Nairobi.

Walliman, N. (2011). *Research Methods:* London: Routledge.

Mulokozi, M. M. (1989). *Tanzu za Fasihi Simulizi*, *Mulika* 21,1-24. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Wafula, R. M. (1999). *Uhakiki wa Tamthiliya Historia na Maendeleo yake.* Nairobi: Jomokenyatta Foundation

Wafula, R. M. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomokenyatta Foundation.

Wamitila, K. W. (2002). *Misingi ya Nadharia ya Fasihi*. (Chapa ya Pli). Nairobi: Video Muwa Publications Ltd.

——— (2010). *Kanz ya Fasihi 1*: *Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi.* Nairobi: Vide Muwa Publications Ltd.

# VIAMBATISHO

## KIAMBATISHO Na. I

## MWONGOZO WA MASWALI YA USAILI KWA AJILI YA WAZEE WANAOISHI KATIKA NYUMBA ZA VIJIJI

Mpendwa,

Ninafanya utafiti unaohusu Kuchunguza Semi Zilizoandikwa Kwenye Kuta za Nyumbaza Vijiji Kisiwani Pemba**.** Lengo kuu la utafiti huu ni kuzibainisha vipengele vya lugha na namna zinavyoibua dhamira mbalimbali.

Kumbuka taarifa zote zitakazotolewa zitahifadhiwa kama siri baina ya mtafiti na mshiriki na pia zitatumika kwa ajili ya utafiti huu tu, na si vinginevyo.


1. Je, jina lako ni Nani?
2. Je, unazijua semi zlizoandikwa kwenye nyumba za vijiji?
3. Kama `Ndio` Taja semi hizo unazozijua.
4. Je, kuna dhamira zozote zinazojitokeza katika semi hizo?
5. Kama NDIO taja dhamira hizo.

**ASANTE KWA USHIRIKIANO WAKO**



**Mtafiti (Upande wa kuchoto mwenye mtandio wenye rangi nyeupe na bluu) akiwa na wakaazi wa nyumba yenye kuchorwa semi za kutani**


TULIYA TU
ISHI WAZU
RIHAWE
SHI?




**Semi katika Ukuta wa Nyumba ya Kijiji**


BURE MNAJIPAZIKI




**Semi katika Ukuta wa Nyumba ya Kijiji**




**Semi katika Ukuta wa Nyumba ya Kijiji**


BURE MNAJIPAZIKI

**Kiambatanisho Na. 3: Semi zilizochorwa kwenye kuta za nyumba za vijijini kisiwani Pemba**

1. Enyi walimwengu usilolijuwa litawasumbua
2. Pita na zako
3. Mchawi house
4. Ngombe wa mchungawe hufungwa na ubingwawe
5. Mwisho wa wimbi ni joma
6. Akupani
7. Ahaeshindanishwa na mungu utamshinda
8. Lishakisaliti kidole na jiwe liwalo lolote na liwe
9. Nasi hula
10. Nyumba ya bilisi
11. Mungu mkubwa
12. Maisha siri
13. Mafumbo yenu ya chuki kwamba mm sishituki
14. Usimuogope mbwa mwenye meno muogope jirani mwenye maneno
15. Nilijuwa roho zitawauma
16. Ukimnunia jirani uombe chumvi kwa nani
17. Kama mm mbaya mwema ni nani
18. Sigogo wala si shina matawi ndiyo fitina
19. Utajiju
20. Wache waseme
21. Usilolijua litakusumbua
22. Mtaka cha mvunguni sharti ainame

23. Mahari yapunguzwe
24. Ilove you
25. Tulia tuishi wazuri haweshi
26. Ndege wangu karudi tunduni
27. Nimebaki na huzuni
28. Jirani msafie nia mola si hiyana atakulipia
29. Usijaze masusu kwa mambo yasiyokuhusu
30. Sema nao cheka nao kusema ndio kazi zao
31. Bure munajipa dhiki kujikwaa na vizingiti
32. Ukipendwa pendeka
33. Kufa lazima
34. Kila uonalo wasema na pia hili kaseme
35. Mbaya halisi na wema hakosi
36. Nuna wewe tu
37. Usinunie sisimizi sukari simalizi
38. Ukiona vyaelea ujuwe vimeundwa
39. Usilolijua litakusumbua
40. Mtaka cha mvunguni sharti ainame
41. Bora adui shetani kama adui kiumbe
42. Wazuri haweshi
43. Nilijuwa roho zitawauma
44. Mafumbo ya chuki kwangu mimi sitaki
45. Utamaliza mtama kunguru hawi njiwa
46. Aljazera halua

47. Haji kiua na haji chandarua banning cd
48. Sapuka na zantel
49. Easy na eze pesa
50. Laki si pesa
51. Mimi ni wako mwengine hatatokea
52. Usimuonee wivu jirani
53. Haki ya mtu haiipotei
54. Haki haizami huelea
55. Malipo ni duniani akhera kwenda hesabu
56. Aisifue mvua imemnyea
57. Alipangalo jalali hakuna wa kupingua
58. Akenda juu kipungu hafikilii mbinguni
59. Hasidi hana sababu
60. Wema hauozi
61. Usijaze masusu kwa mambo yasiyokuhusu
62. Pilipili usiyoila inakuwashia nini
63. Bora moja shika kuliko kumi nenda uje
64. Umenisaliti kidole na jiwe liwalo lolote na liwe
65. Nainyeshe tujuwe pavujapo
66. Hamad kimbindoni
67. Zimwi likujualo halikuli likakwisha
68. Palipo naupendo mungu yupo
69. Kijuwa ndiyo hiki usipouwanika utaula mbichi
70. Leo ni siku ya furaha

71. Funika kombe mwanaharamu apite

72. Usipoziba ufa utajenga ukuta

73. Ukitaka uonekane mbaya dai chako

74. Ndege mjanja hunasa kwa tundo bovu

75. Huu ndiyo uwezezo wetu

76. Majungu yenu mbolea kwangu

77. Kikulacho kinguoni mwako

78. Mzarau mwiba humchoma

79. Jembe halimtupi mkulima

80. Wabaya si wote

81. Mvumilivu hula mbivu

82. Mwenda tenzi na omo hurejea ngamani

83. Mpanda ngazi hushuka

84. Wapambe nuksi

85. Nenda mwana kwenda

86. Fitina titi la paka halifai kukamwa

87. Watende wao

88. Fitina ngozi ya paka haifai kuambwa

89. Kilio cha kusingizia hakina hakina mahozi wala matanga

90. Ndege mjanja hunasa katika tundu bovu

91. Turufu huenda kwa mchezaji

92. Mtu huchuma juani akala kivulini

93. Ndiyo hao

94. Asiye matendo hula uvundo

95. Kula uhondo kwataka matendo

96. Asiyekuja hakuthamini

97. Kilimo kwanza

98. Bahati ya mwenzio usiilalie mlango wazi

99. Kibaya huwa kizuri

100. Kibaya huwa kizuri

101. Silaiki ya mwanadamu huwa kama ngombe

102. Msiba wa kujitakia hauna kilio

103. Maisha ni safari

104. Hulka njema ni sawa na mali

105. Uzuri wa mtu ni tabia